BARAZA LA MITIHANI LA TANZANIA

# TAARIFA YA UCHAMBUZI WA MAJIBU YA WATAHINIWA WA MTIHANI WA UALIMU DARAJA LA A (GATCE) 2018

## 634 STADI ZA KAZI

**BARAZA LA MITIHANI LA TANZANIA**

# TAARIFA YA UCHAMBUZI WA MAJIBU YA WATAHINIWA UALIMU DARAJA LA A (GATCE) 2018

# 634 STADI ZA KAZI

*Kimechapishwa na:*
Baraza la Mitihani la Tanzania,
S.L.P 2624,
Dar es salaam, Tanzania.

**© Baraza la Mitihani la Tanzania, 2018**

Haki zote zimehifadhiwa.

## YALIYOMO

DIBAJI ....................................................................................................................iv

1.0 UTANGULIZI ........................................................................................ 1

2.0 UCHAMBUZI WA UFAULU WA WATAHINIWA KWA KILA SWALI........................................................................................... 2

2.1 Sehemu A ............................................................................................ 2
2.1.1 Swali la 1............................................................................................. 2
2.1.2 Swali la 2............................................................................................. 4
2.1.3 Swali la 3............................................................................................. 6
2.1.4 Swali la 4............................................................................................. 9
2.1.5 Swali la 5........................................................................................... 12
2.1.6 Swali la 6........................................................................................... 15
2.1.7 Swali la 7........................................................................................... 17
2.1.8 Swali la 8........................................................................................... 20
2.1.9 Swali la 9........................................................................................... 23
2.1.10 Swali la 10......................................................................................... 26
2.2 Sehemu B .......................................................................................... 28
2.2.1 Swali la 11......................................................................................... 28
2.2.2 Swali la 12......................................................................................... 32
2.2.3 Swali la 13......................................................................................... 37
2.3 Sehemu C .......................................................................................... 41
2.3.1 Swali la 14......................................................................................... 41
2.3.2 Swali la 15......................................................................................... 45
2.3.3 Swali la 16......................................................................................... 50

3.0 UCHAMBUZI WA KIWANGO CHA UFAULU WA WATAHINIWA KATIKA MADA ............................................ 57

4.0 HITIMISHO........................................................................................ 57

5.0 MAPENDEKEZO............................................................................... 58

Kiambatisho............................................................................................... 60

# DIBAJI

Baraza la Mitihani la Tanzania linayo furaha kutoa taarifa ya watahini kuhusu ufaulu wa watahiniwa wa Mtihani wa Kuhitimu Ualimu Daraja la Tatu A kwa somo la Stadi za Kazi. Taarifa hii imeandaliwa ili kutoa mrejesho wa ufaulu katika mitihani kwa wanachuo, wakufunzi, waandaaji sera na wadau wa elimu kwa ujumla.

Taarifa hii ni tathmini ya mwisho ambayo pamoja na mambo mengine, inaonesha mafanikio katika ufundishaji na ujifunzaji wa somo la Stadi za Kazi. Kimsingi majibu ya watahiniwa ni uthibitisho wa kipi mfumo wa elimu uliweza au ulishindwa kuwapa watahiniwa wawapo katika mafunzo ya Ualimu katika daraja hili.

Uchambuzi uliowasilishwa katika taarifa hii una lengo la kuchangia katika kuelewa zaidi sababu za watahiniwa kufanya vizuri au vibaya katika mtihani wao. Mrejesho huu utawawezesha viongozi wa elimu, viongozi wa vyuo, wakufunzi na wanavyuo kupata mbinu muafaka katika kuboresha ufaulu wa watahiniwa katika mitihani ijayo inayoendeshwa na Baraza la Mitihani la Tanzania.

Baraza la Mitihani la Tanzania litapenda kupokea maoni na mapendekezo kutoka kwa wakufunzi, wanavyuo na umma kwa ujumla ambayo yatatumika katika kuboresha taarifa za watahini zitakazofuata.

Mwisho Baraza linapenda kuwashukuru Maafisa Mitihani, Wakufunzi wa somo na wengine wote walioshiriki katika uchambuzi wa takwimu na kuandaa taarifa hii.

Dkt. Charles E. Msonde
**KATIBU MTENDAJI**

# 1.0 UTANGULIZI

Mtihani wa somo la **634 Stadi za Kazi** kwa watahiniwa wa daraja A (GATCE) ulifanyika Mei 2018 na ulizingatia muhtasari wa somo la Stadi za Kazi wa mwaka 2009. Mtihani huu ulikuwa na sehemu tatu: A, B na C ambapo sehemu A ilikuwa na maswali 10 yaliyokuwa ya lazima kwa watahiniwa wote. Maswali katika sehemu A yalihitaji majibu mafupi na yalihusisha taaluma na ufundishaji. Sehemu B ilikuwa na maswali 3 yenye kupima taaluma peke yake. Katika sehemu hii mtahiniwa alitakiwa kujibu maswali 2 tu. Sehemu C pia ilikuwa na maswali 3 yaliyopima eneo la ufundishaji na katika sehemu hii mtahiniwa alitakiwa kujibu maswali 2 tu. Mtihani wote ulikuwa na alama 100 zilizotawanywa katika sehemu A, B na C. Sehemu A ilikuwa na alama 40, sehemu B na C zilikuwa na alama 30 kila moja.

Ufaulu kwa watahiniwa katika mtihani wa Stadi za Kazi kwa mwaka 2018 ulikuwa wa kiwango kizuri ambapo asilimia **99.92** ya watahiniwa wote waliofanya mtihani walipata wastani wa alama 40 na zaidi. Ufaulu huu umejikita katika viwango vitatu ambavyo ni “vizuri", "wastani" na "hafifu". Ufaulu wa kiwango kizuri ni kuanzia alama 70 hadi 100; kiwango cha wastani ni kuanzia alama 40 hadi 69; na ufaulu wa kiwango hafifu ni kuanzia alama 0 hadi 39. Aidha, chati za viwango vya kufaulu zimeambatishwa ili kufafanua ufaulu wa watahiniwa ambapo rangi ya kijani inawakilisha ufaulu wa kiwango kizuri, rangi ya njano inawakilisha ufaulu wa kiwango cha wastani na ufaulu wa kiwango hafifu unawakilishwa na rangi nyekundu.

Taarifa hii inachambua maswali yaliyojibiwa vizuri, wastani na hafifu ili kuongeza kiwango cha ufanisi katika ufundishaji na ujifunzaji wa somo la Stadi za Kazi. Lengo la uchambuzi huu ni kuonesha hali halisi ya jinsi watahiniwa walivyojibu maswali katika mtihani wa somo la Stadi za Kazi. Sampuli za majibu yao zimeambatanishwa ili kuonesha kilichotarajiwa kufanywa na watahiniwa na kile kilichofanywa. Aidha, taarifa hii pia inaonesha sababu zilizowafanya watahiniwa wengi kupata ufaulu mzuri na wachache kupata ufaulu wa chini katika majibu ya maswali kwa baadhi ya mada. Hivyo, uchambuzi huu umeweka mpango mkakati wa kuimarisha ufundishaji na ujifunzaji wa somo la Stadi za Kazi kwa mada ambazo ufaulu ulikuwa hafifu ili kuinua kiwango cha ufaulu wa mitihani yote inayoendeshwa na Baraza la Mitihani la Tanzania kwa miaka itakayofuata.

Inategemewa kuwa matokeo ya uchambuzi huu yatawanufaisha wanachuo, wakufunzi, waandaaji wa sera na wadau wote wa elimu kwa ujumla.


## 2.0 UCHAMBUZI WA UFAULU WA WATAHINIWA KWA KILA SWALI

### 2.1 Sehemu A

Sehemu A ilikuwa na maswali 10 ya lazima kutoka mada mbalimbali ambapo viwango vya ufaulu kwa maswali ya sehemu hii ilikuwa kama ifuatavyo: Ufaulu mzuri ulikuwa wa alama 03 hadi 04, alama 02 hadi 2.5 ufaulu wa wastani na alama 00 hadi 1.5 ufaulu hafifu. Kila swali katika sehemu hii lilikuwa na jumla ya alama 04.

#### 2.1.1 Swali la 1


Swali lilitoka katika mada ya *Usanii wa Picha, Chapa, Maumbo na Mapambo*. Swali lilimtaka mtahiniwa kutaja njia nne zinazotumika kuhifadhia picha na mapambo mbalimbali katika somo la Stadi za Kazi. Jumla ya watahiniwa 4843 (100%) walifanya swali hili, ambapo watahiniwa 4181 (86.3%) walipata alama 03 hadi 04, watahiniwa 429 (8.9%) walipata alama 02 hadi 2.5 na watahiniwa 233 (4.8%) walipata alama 00 hadi 1.5. Uchambuzi wa majibu ya watahiniwa katika swali hili na ufaulu wao kiasilimia umewasilishwa vizuri katika Chati Na. 1 kwa kuonesha ufaulu wa kiwango hafifu, wastani na kizuri.




**Chati Na. 1:** *Ufaulu wa Watahiniwa kwa Asilimia (%)*

Watahiniwa 4181 (86.3%) waliopata alama 03 hadi 04 waliweza kutaja njia zinazoweza kutumika kuhifadhia picha na mapambo mbalimbali katika somo la Stadi za Kazi kama vile: *Kuhifadhi kwenye masanduku*, *kuhifadhi kwenye maboksi*, *kutundika ukutani* na *kuhifadhi kwenye kabati*. Watahiniwa hao walionesha kuwa na maarifa ya kutosha katika mada husika na waliweza kukidhi matakwa ya swali. Kielelezo 1.1 kinaonesha jibu la mtahiniwa aliyejibu swali hili kwa usahihi.

**Kielelezo 1.1**




1 (i) Kutundika Ukutani
(ii) Kuhifadhi kwenyo kabati
(iii) Kuhifadhi kwenyo Maboksi
(iv) Kuhifadhi katike Masanduku

Kielelezo 1.1 ni sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyejibu vizuri kwa kutaja njia zote nne zinazoweza kutumika kuhifadhia picha na mapambo mbalimbali katika katika somo la stadi za kazi.

Aidha, watahiniwa 429 (8.9%) waliopata ufaulu wa wastani wa alama 02 hadi 2.5 walitoa majibu ambayo hayakujitosheleza katika baadhi ya vipengele na hivyo kupata alama pungufu. Baadhi yao walichanganya vipengele sahihi na visivyo sahihi. Mfano, mtahiniwa pamoja na kutaja hoja sahihi alichanganya na hoja zisizo sahihi kama vile: *Kutupa picha na mapambo yaliyoonekana kuchakaa na kupitwa na wakati*, *kuwauzia wasiojua kutengeneza* jambo lililopelekea kupata alama za wastani.

Kwa upande mwingine, watahiniwa waliopata ufaulu hafifu wengi wao walishindwa kuelewa matakwa ya swali na wengine walionesha kutokuwa na maarifa ya kutosha katika mada husika. Mfano, mtahiniwa alibainisha kanuni za uchoraji picha kama vile: *Michoro ya picha*, *mwanga na kivuli*, *mwonekano wa picha* na *unamu* badala ya kubainisha njia zinazoweza kutumika kuhifadhia picha na mapambo. Kielelezo 1.2 ni sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyeshindwa swali hili.

**Kielelezo 1.2**




01. (i) Michoro ya Picha
(ii) Murange na Kivuli
(iii) Persepective (Muonekano wa Picha).
(iv) Uramu.

Kielelezo 1.2 ni sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyeshindwa kutaja vipengele vyote vinne ambapo alitakiwa kujibu kwa kutaja njia kama vile: Kutandika au kuning'iniza ukutani, kuviringwa na kuning'inizwa juu na kuhifadhi kwenye bahasha au vihifadhio vya kisasa.

### 2.1.2 Swali la 2

Swali lilitoka katika mada ya *Sanaa za Maonyesho*. Swali lilikuwa na sehemu mbili (a) na (b). Katika sehemu (a) mtahiniwa alitakiwa kufasili dhana ya majigambo na katika sehemu (b) mtahiniwa alitakiwa kufafanua kwa ufupi faida mbili za majigambo katika jamii. Kati ya watahiniwa 4843 waliofanya mtihani, watahiniwa 1950 (40.3%) walipata alama 03 hadi 04, watahiniwa 2005 (41.4%) walipata alama 02 hadi 2.5 na watahiniwa 233 (18.3%) walipata alama 00 hadi 1.5. Chati Na. 2 inaonesha ufaulu wa watahiniwa kwa kiwango hafifu, wastani na kizuri.




**Chati Na. 2:** *Ufaulu wa Watahiniwa kwa Asilimia (%)*

Watahiniwa 2005 (41.4%) waliopata ufaulu wa wastani, walitoa majibu ambayo hayakujitosheleza kwa baadhi ya vipengele na hivyo kupata alama pungufu. Baadhi yao walichanganya dhana sahihi na zisizo sahihi. Uchambuzi ulionesha kuwa, walikuwepo watahiniwa walioweza kutaja faida mbili za majigambo katika jamii lakini walishindwa kutoa maana ya dhana majigambo. Wengine waliweza kutoa maana ya dhana ya majigambo na kushindwa kutoa faida za majigambo katika jamii. Kwa mfano, mtahiniwa alitaja faida kama vile: *Majigambo husababisha uhasama kwenye jamii*, *majigambo huharibu haiba ya mtu anayejigamba kwenye jamii kwani jamii huhisi ndiyo tabia yake halisi*, majibu yaliyoonekana kuwa kinyume na faida za majigambo katika jamii.

Aidha, watahiniwa waliopata alama 03 hadi 04 waliweza kufasili kwa usahihi dhana ya majigambo kama *sanaa ya kujisifu au kutamba mbele ya hadhira* na pia walifafanua kwa ufupi faida za majigambo katika jamii kama vile: *kuburudisha jamii*, *kurithisha amali za jamii*, *kuelimisha jamii*, *kuionya jamii*, *kukuza lugha* na *chanzo cha ajira kwa watambaji*. Kielelezo 2.1 ni sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyeweza kujibu swali hili.


**Kielelezo 2.1**

| | |
|---|---|
| 2.(a) | Majigambo ni tawi la fasihi simulizi ambalo wahusika wake huonyesha namna fulani ya kujisifia au kujiona kuwa wao ni bora zaidi. |
| b i/ | Huelimisha jamii; Pale mtu anapoona jamii fulani inajisifia kwa kufanya mambo mazuri kuliko wengine na kuwafanya wengine wawe na chachu zaidi |
| ii/ | Kuburudisha jamii; Samii inapoona michezo kama hii inachezwa watu wengi huwa wanaji-tokeza kwenda kuangalia hiyo michezo na kufulahi zaidi. |

Kielelezo 2.1 ni sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyeweza kueleza dhana ya majigambo na kutoa faida za majigambo katika jamii.

Kwa upande mwingine, watahiniwa 888 (18.3%) waliopata ufaulu hafifu, walionekana kukosa maarifa kuhusu mada ya *Sanaa za Maonyesho* hali iliyopelekea kushindwa kufasili kwa usahihi dhana ya majigambo na pia kushindwa kubaini faida za majigambo katika jamii. Mfano, mtahiniwa alishindwa kutoa maana sahihi ya dhana ya majigambo na kuelezea aina za sifa zinazotumika katika kujigamba jukwaani badala ya kuelezea faida za majigambo katika jamii kama inavyoonekana katika Kielelezo 2.2.

**Kielelezo 2.2**





Kielelezo 2.2 kinaonesha jibu la mtahiniwa aliyeshindwa kufasili kwa usahihi dhana ya majigambo na kushindwa kabisa kuelezea faida za majigambo katika jamii.

### 2.1.3 Swali la 3

Swali lilitoka kwenye mada ya *Ushoni wa Nguo* na lilimtaka mtahiniwa kubaini faida nne za uvaaji wa nguo kwa binadamu. Jumla ya watahiniwa 4843 (100%) walifanya swali hili, ambapo watahiniwa 4753 (98.1%) walipata alama 03 hadi 04, watahiniwa 64 (1.3%) walipata alama 02 hadi 2.5 na watahiniwa 26 sawa na (0.5%) walipata alama 00 hadi 1.5. Uchambuzi wa majibu ya watahiniwa katika swali hili na ufaulu wao


kiasilimia umewasilishwa vizuri katika Chati Na. 3 kwa kuonesha ufaulu wa kiwango hafifu, wastani na kizuri.




**Chati Na. 3:** *Ufaulu wa Watahiniwa kwa Asilimia (%)*

Watahiniwa 4753 (98.1%) waliopata ufaulu mzuri kwa kupata alama 03 hadi 04 waliweza kueleza kwa usahihi faida za kuvaa nguo kwa binadamu. Watahiniwa hao walionekana kuwa na maarifa ya kutosha kuhusu mada ya *Ushoni wa Nguo* na walizingatia matakwa ya swali kwa kuandika faida za kuvaa nguo kama vile: *kuukinga mwili na baridi hasa sehemu zenye baridi*, *mvaaji kuonekana nadhifu*, *kustiri mwili* na *kuonesha utamaduni wa jamii fulani.* Kielelezo 3.1 ni sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyeweza kutoa majibu sahihi katika swali hili.

**Kielelezo 3.1**




3. i) Husaidia kujikinga dhidi ya baridi kali kwa sababu hufunika ngozi
ii) Husaidia kusitiri mili zetu kuepuka ku tembea uchi
iii) Hutufanya tuonekane nadhifu wakati wote
iv) Husaidia kujikinga na jua kali wakati wa mchana.

Kielelezo 3.1 kinaonesha jibu la mwanafunzi aliyeweza kutaja faida zote nne za kuvaa nguo kwa binadamu kwa usahihi.

Aidha, watahiniwa 64 (1.4%) waliopata ufaulu wa wastani walitoa majibu ambayo hayakukidhi mahitaji ya swali. Baadhi yao walichanganya hoja sahihi na zisizo sahihi. Mfano, pamoja na kuandika hoja sahihi, mtahiniwa alichanganya na hoja zisizo sahihi kama vile: *Kuonesha umaarufu, kuvaa nguo za heshima* majibu yaliyosababisha kupata alama za wastani.

Kwa upande mwingine, pamoja na ufaulu mzuri wa watahiniwa walio wengi katika swali hili, watahiniwa 26 sawa na asilimia 0.5 walipata alama hafifu. Uchambuzi unaonesha kuwa, watahiniwa hao walikosa maarifa kuhusu mada husika na walishindwa kuelewa matakwa ya swali. Mfano, mtahiniwa alifasili swali vibaya badala ya kutaja faida za kuvaa nguo aliandika faida za kufua nguo kama vile: *Kuondoa uchafu ulioko kwenye nguo, kuondoa harufu mbaya* n.k. Hata hivyo mtahiniwa huyo alikosea kwa kuandika faida za kuvua nguo badala ya kufua nguo kama inavyoonekana katika Kielelezo 3.2.


**Kielelezo3.2**


3. Kubainisha faida nne za uvaaji wa nguo kwa binadamu.
(i) Kuondoa uchafu uliopo katika nguo
(ii) Kuondoa vijidudu kwa kuua ~~kwa~~ nguo kwa kutumia maji ya moto.
(iii) Kuondoa harufu mbaya katika nguo.

Kielelezo 3.2 ni sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyeshindwa kubainisha faida nne za uvaaji nguo ambapo alitakiwa kujibu kwa kutaja faida kama vile: Hutambulisha utamaduni wa jamii fulani, huukinga mwili na baridi kali, zinaustiri mwili na kumfanya mvaaji kuwa nadhifu.

## 2.1.4 Swali la 4


Swali lilitoka kwenye mada ya *Upishi*. Swali lilimtaka mtahiniwa kuelezea kwa kifupi njia nne zinazoweza kutumika kufundishia mada ya Upishi kwa wanafunzi wa Darasa la Tano. Jumla ya watahiniwa 4843 (100%) walifanya swali hili, ambapo watahiniwa 2840 (58.6%) walipata alama 03 hadi 04, watahiniwa 903 (18.7%) walipata alama 02 hadi 2.5 na watahiniwa 1100 (22.7%) walipata alama 00 hadi 1.5. Chati Na. 4 inafafanua viwango vya ufaulu katika swali hili.




**Chati Na. 4:** *Ufaulu wa Watahiniwa kwa Asilimia (%)*

Watahiniwa waliopata alama kati ya 03 hadi 04 waliweza kuelezea kwa kifupi njia zinazoweza kutumika kufundishia mada ya *Upishi* kwa wanafunzi wa Darasa la Tano kwa kutoa hoja kama vile: *Mbinu ya ziara*, *majadiliano*, *maswali na majibu*, *kualika mgeni*, *onesho mbinu* na *igizo dhima*. Watahiniwa hao walionesha kuwa na maarifa ya kutosha katika mada husika na waliweza kukidhi matakwa ya swali. Kielelezo 4.1 kinaonesha jibu la mtahiniwa aliyejibu swali hili kwa usahihi.

**Kielelezo 4.1**


4. Zifuatazo ni njia zinazoweza kutumika katika kufundishia mada ya upishi.

i/ Majadiliano ya vikundi

- Hii ni njia ambayo mwalimu anatakiwa kufundisha upishi kwa kugonganisha mawazo ya wanafunzi pamoja namna ya kupika vyakula mbalimbali

ii/ Onesho mbinu.

- Ni njia ambayo mwalimu anatakiwa kufanya yeye mwenyewe kitendo au vitendo vya upishi ili wanafunzi waige.

iii/ Igizo dhima

- Mwalimu anatakiwa awe na utaalamu wa kutumia igizo dhima kwa kuandaa wahusika watakao onesha njinsi ya kufanya maandalizi ya upikaji.

iv/ Kisa mafunzi


- Mwalimu hapa hutakiwa kuandaa simulizi ambayo inahusiana na upishi baadae aulize maswali ya kuhusiana na upishi uliojitokeza kwenye kisa hicho.

Kielelezo 4.1 ni sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyejibu vizuri kwa kueleza kwa kifupi njia nne zinazoweza kutumika kufundishia mada ya Upishi kwa wanafunzi wa Darasa la Tano.

Aidha, watahiniwa 903 waliopata alama 02 hadi 2.5 walitoa majibu ambayo hayakujitosheleza katika baadhi ya vipengele na hivyo kupata alama pungufu. Baadhi yao, walichanganya vipengele sahihi na visivyo sahihi. Mfano, mtahiniwa baada ya kutaja njia mbili sahihi alichanganya na zisizo sahihi kama vile: *wanafunzi kutunza kumbukumbu ya kudumu* na *wanafunzi kufurahia somo* kana kwamba sehemu ya swali ilimhitaji kutaja faida za kutumia mbinu fulani ya kufundishia na kujifunzia.

Kwa upande mwingine, watahiniwa 1100 (22.7%) waliopata ufaulu hafifu baadhi yao walishindwa kuelewa matakwa ya swali na wengine walionesha kutokuwa na maarifa ya kutosha katika mada husika. Mfano, mtahiniwa alieleza njia nne zinazotumika kupika vyakula kama vile: *njia ya kuoka, kukaanga, kuchemsha, kuchoma*. Vile vile mtahiniwa mwingine alieleza hatua za kufuata katika mapishi ya ugali kama vile: *kuandaa moto*, *kuandaa sufuria*, *kuchemsha maji kisha kuweka unga na kusonga ugali* badala ya njia zinazoweza kutumika kufundishia mada ya Upishi. Kielelezo 4.2 ni sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyeshindwa swali hili.

**Kielelezo 4.2**




4\. 1. Kuoka: Hii ni njia ya kupika chakula bila kugusana na moto wa maji mfano mikate, skonzi, keki
2. Kukaanga: Hii ni njia ya kupika chakula kwa kutumia mafuta bila kuweka maji mfano chapati, maandazi
3. Kuchemsha: Hii ni njia ya kupika chakula kwa kukiweka katika sufuria na kuweka maji kiasi na kubandika kwenye jiko mfano viazi na mihogo
4. Kuchoma: Hii ni njia ya kupika chakula bila kukiweka kwenye chombo kama sufuria hupikwa kwa kuwekwa juu ya waya na mkaa kwa chini.

Kielelezo 4.2 ni sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyeelezea njia nne zinazotumika kupika vyakula badala ya kuonesha njia za kufundishia mada ya upishi kwa wanafunzi wa Darasa la Tano. .

### 2.1.5 Swali la 5

Swali hili lilitoka katika mada ya *Misingi ya Kufundisha Somo la Stadi za Kazi*. Swali lilimtaka mtahiniwa kutaja mambo manne yanayofanya kuwepo kwa usawa wa kijinsia katika ufundishaji. Jumla ya watahiniwa 4843 (100%) walifanya swali hili, ambapo watahiniwa 1881 (38.8%) walipata alama 03 hadi 04, watahiniwa 1565 (32.4%) walipata alama 02 na


2.5 na watahiniwa 1397 sawa na 28.8% walipata alama 00 hadi 1.5. Chati Na. 5 inawasilisha ufaulu wa watahiniwa kwa asilimia.




**Chati Na. 5:** *Ufaulu wa Watahiniwa kwa Asilimia (%)*

Watahiniwa waliopata alama kati ya 03 hadi 04 waliweza kuorodhesha kwa usahihi mambo yanayofanya kuwepo kwa usawa wa kijinsia katika ufundishaji kama vile: *mgawanyo sawa wa madaraka katika uongozi na makundi ya kimasomo*, *ushiriki sawa katika michezo*, *utoaji ulio sawa wa adhabu* na *ushirikishwaji wa jinsia zote katika tendo zima la ufundishaji na ujifunzaji*. Watahiniwa hao walionesha kuwa na maarifa ya kutosha katika mada husika na waliweza kukidhi matakwa ya swali. Kielelezo 5.1 kinaonesha jibu la mtahiniwa aliyejibu swali hili kwa usahihi.

**Kielelezo 5.1**





Kielelezo 5.1 ni sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyejibu vizuri kwa kutaja mambo yanayofanya kuwepo kwa usawa wa kijinsia katika ufundishaji kama swali lilivyohitaji.

Aidha, watahiniwa waliopata alama 02 hadi 2.5 katika swali hili, walitoa majibu ambayo hayakujitosheleza kwa baadhi ya vipengele na hivyo kupata alama pungufu. Baadhi yao walichanganya vipengele sahihi na visivyo sahihi. Mfano, mtahiniwa alichanganya hoja zisizo sahihi kama vile: *Kuwashirikisha kikamilifu wakati wa kuuliza maswali kwa wanafunzi* bila kuonesha kwa usahihi ni kina nani wanaopaswa kushirikishwa, *kuwapa wote kazi za kuosha vyombo na kukata kuni*, majibu yaliyoonekana kutojitosheleza na hivyo kupata alama za wastani.

Kwa upande mwingine, watahiniwa waliopata alama 00 hadi 1.5 baadhi yao, walishindwa kuelewa matakwa ya swali na wengine walionesha kutokuwa na maarifa ya kutosha katika mada husika. Pamoja na hayo, kati yao walionekana kuchanganya maarifa. Mfano, mtahiniwa alitaja *maendeleo ya sayansi na teknolojia, utandawazi, mahitaji ya jamii, kuondokana na*

*umaskini* kama mambo yanayofanya kuwepo kwa usawa wa kijinsia katika ufundishaji. Kielelezo 5.2 ni sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyeshindwa swali hili kwa kutoa majibu yaliyokuwa hayana uhusiano na swali.

**Kielelezo 5.2**




5. (i) Maendeleo ya Sayansi na teknolojia
(ii) Utandawazi
(iii) Mahitaji ya jamii
(iv) Ili kuondokana na umaskini.

Kielelezo 5.2 ni sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyeshindwa kutoa majibu sahihi katika swali hili ambapo alitakiwa kutoa majibu kama; ushiriki uliosawa katika michezo shuleni, matumizi sahihi ya lugha kwa jinsia zote, mgawanyo sawa wa madaraka katika uongozi kwa jinsia zote n.k.

### 2.1.6 Swali la 6


Swali lilitoka kwenye mada ya *Ufundishaji*. Swali lilimtaka mtahiniwa kufafanua manufaa manne ya ubunifu katika ufundishaji. Jumla ya watahiniwa 4843 (100%) walifanya swali hili ambapo watahiniwa 3555 (73.4%) walipata alama 03 hadi 04, watahiniwa 937 (19.4%) walipata alama 2 hadi 2.5 na watahiniwa 351 (7.2%) walipata alama 00 hadi 1.5 kama inavyoonekana kwenye Chati Na. 6.




**Chati Na. 6:** *Ufaulu wa Watahiniwa kwa Asilimia (%)*

Asilimia 73.4 ya watahiniwa waliopata alama 03 hadi 04 waliweza kueleza kwa ufasaha manufaa ya ubunifu katika ufundishaji kwa kutoa hoja kama: *Humsaidia mwalimu kutengeneza kwa kufaragua zana za kufundishia, humsaidia mwalimu kubuni njia mbalimbali za kufundishia, humsaidia mwalimu kuandaa somo linaloeleweka* pia *humwezesha mwalimu kwenda na mabadiliko yanayotokea kwenye jamii*. Watahiniwa hao walionesha kuwa na maarifa ya kutosha katika mada husika na waliweza kukidhi matakwa ya swali. Kielelezo 6.1 kinaonesha jibu la mtahiniwa aliyeweza kujibu swali hili kwa usahihi.

**Kielelezo 6.1**



6. Ubunifu: ni kitendo cha kufikiri na kuangali na kuanua kufanya au kutengeneza kitu au jambo ambalo halikuwepo. Ufuatao ni umuhimu wa ubunifu katika ufundishaji.

Humsaidia mwalimu kubuni na kubaini mbinu za kufundishia na kujifunzia darasa ni kipindi anapoona wanafunzi wake hawa muelewi.

Humsaidia mwalimu kufaragua na kutengeneza zana za kufundishia na kujifunzia ~~kwa~~ papo kwa papo awapo darasani.

Humsaidia mwalimu kujijenga stadi mbalimbali katika ufundishaji na ujifunzaji wa somo wakati awapo darasani.

Humsaidia mwalimu kujenga kanuni takaro wafanya wanafunzi wawelewe kuelewa somo kwa kuwaaminisha ukweli kuhusu kanuni hizo.


Mwalimu kwenye taaluma ya ualimu aliyepitia na kupata ujuzi huu ni mbunifu katika kutengeneza, kufundisha na kufaragua zana za kufundishia na kujifunzia.

Kielelezo 6.1 ni sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyejibu vizuri kwa kutaja manufaa manne ya ubunifu katika ufundishaji.

Aidha, watahiniwa (19.4%) waliopata ufaulu wa wastani, walitoa majibu ambayo hayakujitosheleza katika baadhi ya vipengele na hivyo kupata alama pungufu. Baadhi yao katika kujibu swali walichanganya vipengele sahihi na visivyo sahihi na wengine walirudia kuandika hoja zaidi ya mara moja. Mfano, mtahiniwa baada ya kutaja mambo mawili sahihi yanayoonesha umuhimu wa ubunifu katika ufundishaji, alichanganya na hoja zingine zisizo sahihi kama vile: *Kujipatia ajira* na *kutengeneza mapambo ya aina mbalimbali* jambo lililosababisha kupata alama za wastani.

Kwa upande mwingine, watahiniwa 351 waliopata ufaulu hafifu baadhi yao walishindwa kuelewa matakwa ya swali na wengine walionesha kukosa maarifa ya kutosha kwenye dhana ya ubunifu katika ufundishaji. Mfano, mtahiniwa aliandika faida za ubunifu katika maisha kwa ujumla kwa kueleza hoja kama: *Kukuza kipato*, *chanzo cha ajira*, *kukabiliana na mazingira* na pia *kupunguza umaskini* badala ya kutaja faida za ubunifu katika ufundishaji kama swali lilivyohitaji. Kielelezo 6.2 ni sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyeshindwa swali hili.

**Kielelezo 6.2**



6 (a) Kukuza kipato
(b) Chanzo cha ajira
(c) Kukabiliana na hali ya mazingira ya aina yeyote.
(d) Kupunguza Umaskini

Kielelezo 6.2 ni sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyetaja faida za ubunifu katika maisha kinyume na matakwa ya swali.

### 2.1.7 Swali la 7

Swali lilitoka katika mada ya *Muziki* na lilimtaka mtahiniwa kueleza maana ya istlahi *mwafaka*, *ridhimu*, *kilele* na *kigao* kama zinavyotumika kwenye fani ya *Muziki*. Jumla ya watahiniwa 4843 (100%) walifanya swali hili, ambapo watahiniwa 3965 (81.9%) walipata alama 00 hadi 1.5, watahiniwa


603 (12.4%) walipata alama 02 hadi 2.5 na watahiniwa 275 (5.7%) walipata alama 03 hadi 04 kama inavyoonekana katika Chati Na. 7.




**Chati Na. 7:** *Ufaulu wa Watahiniwa kwa Asilimia (%)*

Watahiniwa wengi (81.9%) waliopata alama 00 hadi 1.5 walishindwa kueleza maana ya dhana *mwafaka*, *ridhimu*, *kilele* na *kigao* kwa ufasaha kama zinavyotumika katika Muziki. Wengi kati yao walionesha kutokuwa na maarifa kabisa katika kueleza dhana hizo. Mfano, mtahiniwa mmoja alichanganya dhana hizo na vifaa vya muziki, alieleza maana ya mwafaka kama *kifaa kinachotumika kurekodia mapigo ya sauti katika muziki* wakati mtahiniwa mwingine alitoa maana ya dhana hizo kama zinavyotumika katika maisha ya kila siku. Mtahiniwa huyo alieleza dhana ya mwafaka kama ni *hali ya watu wawili kukubaliana kwenye mazungumzo.* Kielelezo 7.1 ni sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyeshindwa swali hili.

**Kielelezo 7.1**


(a) Mwafaka
ni hali ya kufikia kiwango fulani cha uelewano
juu ya kile ambacho kilikuwa
kinazungumziwa na wazungumzaji hao
b) Ridhimu.
ni kitendo cha mtu kurithia na kukubali
kitu ambacho wamezungumza na mtu fulani
c) Kilele
ni hali ya kufikia mwisho wa makubaliano
au jambo fulani linapofanyika.
d) Kigao
ni kitaa au kitu kinachogawanya vitu vingine
mara moja au zaidi ya moja.

Kielelezo 7.1 ni sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyetoa maana ya dhana Mwafaka, Ridhimu, Kilele na Kigao kama zinavyotumika katika maisha ya kila siku kinyume na matakwa ya swali.

Aidha, watahiniwa waliopata ufaulu wa wastani walitoa maana ambazo hazikuwa sahihi kwa baadhi ya istilahi zilizoulizwa. Baadhi yao waliweza kutoa maana sahihi kwa kipengele (a) na (b) na walishindwa kujibu vipengele vingine kwa usahihi jambo lililopelekea kupata alama za wastani.

Kwa upande mwingine, watahiniwa 275 (5.7%) waliopata ufaulu mzuri katika swali hili, waliweza kueleza maana ya dhana zilizoulizwa kama zinavyotumika kwenye fani ya Muziki. Mfano mtahiniwa alieleza dhana ya *mwafaka ni mpangilio wa solfa za muziki ili kuleta uzuri wa wimbo, ridhimu ni mwendo linganifu wa mapigo ili kulingana/kwenda na ghani*, *kilele ni kiwango cha mfiko wa sauti kuwa juu sana au chini sana* na *kigao ni mstari unaotenga vigao vya ridhimu au muziki*. Watahiniwa hao walionesha kuwa na maarifa ya kutosha na waliweza kukidhi matakwa ya swali. Kielelezo 7.2 kinaonesha jibu la mtahiniwa aliyejibu swali hili vizuri.

**Kielelezo 7.2**

7. a). Mwafaka. Ni mpangilio sahihi wa Solfa za muziki ambazo huwa zinezingatia kordi (trayadi), Solfa mbili au zaidi zinazosikika pamoja hufanya mwafaka kuwa linganifu mfano wa kordi (Trayadi) ni DO MI SO, REFALA, MISOTI.

b). Ridhimu - Ni mwendo linganifu wa mapigo kuendana na ghani, ridhimu yaweza kuwa katika mwendo wa $\frac{2}{4}, \frac{3}{4}, \frac{4}{4}, \frac{3}{8}, \frac{6}{8}, \frac{5}{8}, \frac{6}{16}, \frac{12}{20}, \frac{16}{34}$ nk.


c). Kilele - Ni mfiko wa pamoja wa sauti ambapo sauti zote hupaswa kumaliza pamoja baada ya kuwepo na mtawanyiko wa sauti zenye kufuata mpangilio wa mapigo na kordi.

d). Kigao - Ni mstari wa wima ambao huweza kugawa wimbo katika hatua mbalimbali Mstari huu hukatika na kuzikata stevu za Muziki. na huwa unagawa wimbo katika mpangilio maalumu wa mapigo.

Kielelezo 7.2 ni sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyejibu swali vizuri kwa kueleza dhana zote nne kwa usahihi kama zinavyotumika kwenye fani ya Muziki.

### 2.1.8 Swali la 8

Swali lilitoka katika mada ya *Ufundishaji*. Swali lilimtaka mtahiniwa kubaini faida nne za kutumia mbinu ya majadiliano katika kufundisha mada ya Biashara Ndogondogo. Jumla ya watahiniwa 4843 (100%) walifanya swali hili ambapo watahiniwa 4686 (96.8%) walipata alama 03 hadi 04, watahiniwa 93 (1.9%) walipata alama 02 hadi 2.5 na watahiniwa 64 (1.3%) walipata alama 00 hadi 1.5. Chati Na. 8 inaonesha kiwango cha ufaulu wa watahiniwa.





**Chati Na. 8:** *Ufaulu wa Watahiniwa kwa Asilimia (%)*

Watahiniwa waliopata alama kati ya 03 hadi 04 waliweza kubaini faida nne au tatu za mbinu ya majadiliano katika kufundishia mada ya *Biashara Ndogondogo* kwa kutoa hoja kama vile:

> Njia ya majadiliano ni njia nzuri ya kupata mawazo mbalimbali kutoka kwa washiriki, hutatua changamoto za ujifunzaji kwa urahisi, husaidia wanafunzi kukuza stadi za ushirikiano, kusikiliza na kujieleza na pia huwafanya wanafunzi kuwa na maamuzi ya busara na kubadilisha mitazamo yao juu ya Biashara Ndogondogo.

Watahiniwa hao walionesha kuwa na maarifa ya kutosha katika mada ya ufundishaji na waliweza kukidhi matakwa ya swali. Kielelezo 8.1 kinaonesha jibu la mtahiniwa aliyejibu swali hili kwa usahihi.

**Kielelezo 8.1**


8. Faida za kutumia mbinu ya majadiliano:

i. Humjengea mwanafunzi kumbukumbu ya kudumu

=> mwanafunzi akijifunza mada ya biashara ndogondogo kwa kujadiliana na wenzake huwa si rahisi kusahau

ii. Humfikirisha mwanafunzi na kumjengea udadisi

=> mwanafunzi akijifunza kwa kutumia majadiliano atafikiria na kuwa mdadisi wa hali ya kujifunza kwani huwa anaona biashara hizo katika maeneo anakotokea.

iii. Humwezesha mwanafunzi kuhusianisha somo na mazingira.

=> mwanafunzi akijifunza mada ya biashara ndogondogo kwa majadiliano atawezakukumbuka mazingira ya nyumbani anakotokea


iv. Humfanya mwanafunzi ashiriki kikamilifu katika somo kwa kutoa mawazo kile ambacho anakifikiria yeye kuhusiana na biashara ndogondogo.

Kielelezo 8.1 ni sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyeweza kueleza faida za mbinu ya majadiliano katika kufundisha mada ya Biashara Ndogondogo kwa usahihi.

Aidha, asilimia 1.9 ya watahiniwa waliopata ufaulu wa wastani walitoa majibu ambayo hayakujitosheleza katika baadhi ya vipengele na hivyo kupata alama za wastani. Mfano, mtahiniwa pamoja na kutoa vipengele viwili sahihi alitaja hoja ambazo si sahihi kama vile: *kusaidia kila mwanafunzi kuelewa somo* na *njia hii hupoteza muda wa kujifunza* na hivyo kupata alama za wastani.

Kwa upande mwingine, watahiniwa 64 (1.3%) waliopata ufaulu hafifu baadhi yao walionesha kutokuwa na maarifa ya kutosha katika mada husika na wengine walishindwa kuelewa matakwa ya swali. Mfano, mtahiniwa mmoja alitaja mbinu tofauti za kufundishia kwa kutoa hoja kama; *maswali na majibu*, *ziara*, *majadiliano* na *kualika mgeni* badala ya kuonesha faida za mbinu ya majadiliano katika kufundishia mada ya Biashara Ndogondogo. Kielelezo 8.2 ni sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyeshindwa swali hili.

**Kielelezo 8.2**




8 (i) Maswali na majibu
(ii) Mbinu ya ziara
(iii) Majadiliano
(iv) Alika mgeni Mfano Mfanyabi-
ashara ndogondogo kama vile machi-
nga.

Kielelezo 8.2 kinaonesha sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyetaja mbinu za kufundishia badala ya faida za mbinu ya majadiliano kama swali lilivyotaka.

### 2.1.9 Swali la 9


Swali lilitoka katika mada ya *Misingi ya Kufundisha Somo la Stadi za Kazi*. Swali lilimtaka mtahiniwa kuonesha umuhimu wa Urazini wa Ujumi katika maisha ya kila siku. Jumla ya watahiniwa 4843 (100%) walifanya swali hili ambapo watahiniwa 3337 (68.9%) walipata alama 03 hadi 04, watahiniwa 608 (12.6%) walipata alama 02 hadi 2.5 na watahiniwa 898 (18.5%) walipata alama 00 hadi 1.5. Chati Na. 9 inaonesha ufaulu wa watahiniwa kwa kiwango hafifu, wastani na kizuri.




**Chati Na. 9:** *Ufaulu wa Watahiniwa kwa Asilimia (%)*

Watahiniwa waliopata alama 03 hadi 04 waliweza kueleza umuhimu wa Urazini wa Ujumi katika maisha ya kila siku kwa kutoa hoja kama: *kujua uzuri wa mazingira*, *kusaidia kuboresha mazingira na jamii*, *kusaidia katika kuhifadhi uoto wa asili* na pia *kuifahamu dunia yetu jinsi ilivyo*. Watahiniwa hao walionesha kuwa na maarifa ya kutosha katika mada ya Misingi ya Kufundisha somo la Stadi za Kazi na waliweza kukidhi matakwa ya swali. Kielelezo 9.1 kinaonesha jibu la mtahiniwa aliyejibu swali hili kwa usahihi.

**Kielelezo 9.1**



9. (i) Msingi wa Urazini wa ujumi husaidia kujua uzuri wa mazingira na jinsi ya kuyo hivyo, hii hutokana na kusaidia kujua mazingira halisi
(ii) Husaidia kuboresha mazingira na jamii kwa ujumla ambapo msingi huu unatoa elimu kuhusu mazingira
(iii) Husaidia namna ya kuhifadhi na kutunza uoto asilia wa mazingira kwa pamoja na kutoweka kwa viumbe hai mbalimbali duniani.
(iv) Husaidia kujifahamu dunia jinsi ilivyo na uzuri pamoja viumbe vilivyomo msingi wa urazini na ujumi huweza kujifunza kwa kuzingatia hayo

Kielelezo 9.1 ni sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyeweza kuonesha kwa usahihi umuhimu wa Urazini wa Ujumi katika maisha ya kila siku.

Aidha, asilimia 12.6 ya watahiniwa waliopata ufaulu wa wastani wa alama 02 hadi 2.5 walitoa majibu ambayo hayakujitosheleza kwa baadhi ya vipengele na hivyo kupata alama pungufu. Mfano, mtahiniwa alichanganya hoja zisizo sahihi kama vile: *kupunguza uvivu na uzembe kazini na kukua kwa mtaji* jambo lililopelekea kupata alama za wastani.

Kwa upande mwingine, watahiniwa waliopata ufaulu hafifu walishindwa kuelewa matakwa ya swali na wengine kati yao walionesha kukosa maarifa ya kutosha katika mada husika. Kwa mfano, mtahiniwa alieleza faida za kazi za sanaa katika jamii kwa kutoa hoja kama vile: *Kuburudisha jamii, kuelimisha jamii* na *kuonya jamii* badala ya umuhimu wa Urazini wa Ujumi katika maisha ya kila siku kama invyoonekana katika Kielelezo 9.2.


**Kielelezo 9.2**




Kielelezo 9.2 ni sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyetaja faida za kazi za sanaa kama kuelimisha jamii, kusisimua n.k ambazo ni kinyume na matakwa ya swali.

### 2.1.10 Swali la 10


Swali lilitoka katika mada ya *Kilimo, Ufugaji na Uvuvi*. Swali lilimtaka mtahiniwa kubainisha makundi manne ya mboga kwa kutoa mifano. Kati ya watahiniwa 4843 waliofanya swali hili watahiniwa 2357 (48.7%) walipata alama 03 hadi 04, watahiniwa 822 (16.9%) walipata alama 02 hadi 2.5 na watahiniwa 1664 sawa na 34.4% walipata alama 00 hadi 1.5. Chati Na. 10 inaonesha ufaulu wa watahiniwa kwa kiwango hafifu, wastani na kizuri.




**Chati Na. 10:** *Ufaulu wa Watahiniwa kwa Asilimia (%)*

Watahiniwa waliopata alama kati ya 03 hadi 04 waliweza kubainisha kwa ufasaha na kwa kutoa mifano ya makundi manne au matatu ya mimea ya mboga kwa kutoa hoja zifuatazo: *mboga za majani, mfano mchicha*, *mboga za mizizi, mfano karoti*, *mboga za maua, mfano kouliflower* na *mboga za matunda, mfano nyanya.* Watahiniwa hao walionesha kuwa na maarifa ya kutosha katika mada husika na waliweza kikidhi matakwa ya swali kwa kutaja aina ya kundi la mboga na kuonesha mfano wake. Kielelezo 10.1 kinaonesha jibu la mtahiniwa aliyejibu swali hili vizuri.

**Kielelezo 10.1**



1b i) Mboga za majani
mfano;- mchicha, Kisamvu, matembere.
ii) Mboga za matunda
mfano; Nyanya, hoho, bamia na biringanya
iii) Mboga za mizizi
mfano; Karoti na Kitunguu
iv) Mboga za maua
mfano; Koliflawa


Kielelezo 10.1 ni sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyejibu swali hili vizuri kwa kubainisha kwa usahihi makundi manne ya mboga na mifano yake.

Aidha, watahiniwa waliopata alama 02 hadi 2.5 walitoa majibu ambayo hayakujitosheleza kwenye baadhi ya vipengele. Baadhi waliweza kutaja makundi ya mboga lakini walishindwa kubainisha mifano sahihi kwa kila kundi na hivyo kupata alama pungufu. Wengine walichanganya vipengele sahihi na visivyo sahihi. Mfano, mtahiniwa pamoja na kutoa hoja sahihi alibainisha kuwa *mimea ya mashina* pia ni aina ya mimea ya mboga, ambayo haikuwa sahihi na hivyo, kupata alama za wastani.

Kwa upande mwingine, watahiniwa waliopata ufaulu hafifu wa alama 00 hadi 1.5 walishindwa kuelewa matakwa ya swali na baadhi walionesha kukosa maarifa ya kutosha katika mada hii. Kwa mfano, mtahiniwa alishindwa kubainisha makundi ya mimea ya mboga kwa kutaja aina za mazao mchanganyiko kama vile *maharage*, *mahindi* n.k. Mtahiniwa

mwingine alieleza namna mbalimbali za uoteshaji wa mimea kwa kutoa hoja kama: *mimea ya kumwaga mbegu*, *mimea ya kupandikiza*, *mimea ya kutambaa* n.k kama inavyoonekana katika kielelzo 10.2.

**Kielelezo 10.2**


10 a) Mimea ya kumwaga mbegu
Mfano Mchicha
b) Mimea ya kupandikiza
Mfano Spinachi
c) Mimea ya kutambaa
Mfano Kunde.
d) Mimea ya asili
Mfano: Kisamvu | Kasava.


Kielelezo 10.2 kinaonesha jibu la mtahiniwa aliyetaja aina ya mazao kutegemea yanavyooteshwa badala ya makundi ya mimea ya mboga kama swali lilivyohitaji.

## 2.2 Sehemu B

Sehemu B ya mtihani huu ilikuwa na maswali 3 ambapo mtahiniwa alitakiwa kujibu maswali 2 tu kutoka katika sehemu hii. Kila swali lilikuwa na alama 15. Viwango vya ufaulu kwa maswali ya sehemu B (11 hadi 13) vilikuwa kama ifuatavyo: Ufaulu mzuri ulianzia alama 10.5 hadi 15, ufaulu wa wastani ulianzia alama 06 hadi 10 na ufaulu hafifu ulianzia alama 00 hadi 5.5.

### 2.2.1 Swali la 11


Swali lilitoka kwenye mada ya *Usanii wa picha, Chapa, Maumbo na Mapambo* ambalo lilimtaka mtahiniwa kueleza sababu tano za kuweka urembo kwenye nguo na bidhaa nyingine. Jumla ya watahiniwa 2909 (60.1 %) kati ya 4843 walifanya swali hili, ambapo kati yao watahiniwa 1979 (68%) walipata alama 10.5 hadi 15, watahiniwa 912 (31.4%) walipata alama 06 hadi 10 na watahiniwa 18 (0.6%) walipata alama 00 hadi 5.5. Chati Na. 11 inaonesha ufaulu wa watahiniwa kwa kiwango hafifu, wastani na kizuri.




**Chati Na. 11:** *Ufaulu wa Watahiniwa kwa Asilimia (%)*

Watahiniwa waliopata alama kati ya 10.5 hadi 15 waliweza kueleza kwa usahihi sababu za kuweka urembo katika nguo na bidhaa nyingine kwa kutoa hoja kama vile: *Kuongeza thamani ya nguo na vitu vingine, kupunguza kasi ya kuchakaa kwa vitu au nguo, kupendezesha vitu au nguo, kuvutia wateja* n.k. Watahiniwa hao walionesha kuwa na maarifa ya kutosha katika mada hii na waliweza kikidhi matakwa ya swali kwa kueleza sababu sahihi za kuweka urembo kwenye nguo na bidhaa zingine. Kielelezo 11.1 kinaonesha sehemu ya majibu ya mtahiniwa aliyejibu swali hili kwa usahihi.

**Kielelezo 11.1**



11. Kuweka urembo katika nguo ni kitendo cha kutia nakshi au mapambo mbalimbali katika nguo. mapambo hayo yanaweza kuwa ni maua mbalimbali ambayo yanaweza kuwekwa kwa kutarizi. ni muhimu kuweka urembo kwenye nguo kwa sababu zifuatazo.

Kupendezesha nguo; Nguo inapopambwa huwa na muonekano mzuri na huwa ni ya kuvutia kutokana na mapambo mbalimbali kama vile maua.

Kuithamanisha au kuongezea nguo thamani; nguo inapopambwa au kuwekewa mapambo thamani yake huongezeka hivyo hata gharama ya kununua huongezeka.

Kuimarisha nguo; mfano nguo inapotarizi wa pembeni huweza kuwa imara na yenye kudumu kwa muda mrefu.

Kuwavutia wanunuzi; wateja au wanunuzi wa nguo huvutiwa zaidi na nguo zenye urembo au zilizopambwa.

Kuweza kujiajiri; kuweka urembo kwenye nguo watu hufanya kazi hiyo ili kujiingizia kipato na kuweza kuinua maisha yao kwa ujumla.

Kuweka mapambo au urembo kwenye nguo kumefanya watu wengi kuinua maisha yao kiuchumi kutokana na watu wengi kujiajiri katika kazi ya kuweka mapambo kwenye nguo mfano watu wanatarizi nguo huweza kujiingizia kipato kupitia fursa za urembaji wa nguo.

Kielelezo 11.1 ni sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyejibu vizuri kwa kueleza sababu tano za kuweka urembo kwenye nguo na bidhaa nyingine.

Aidha, watahiniwa waliopata ufaulu wa wastani wa alama 06 hadi 10 walitoa majibu ambayo hayakujitosheleza katika baadhi ya vipengele. Baadhi yao pamoja na kueleza baadhi ya hoja sahihi walichanganya na hoja zisizo sahihi. Wengine mbali na kushindwa kuwa na maelezo yenye kutetea

hoja zao, walishindwa pia kuandika utangulizi kwa usahihi na hivyo kupata alama za wastani.

Kwa upande mwingine, watahiniwa waliopata alama 00 hadi 5.5 walishindwa kuelewa matakwa ya swali na wengine walionesha kukosa maarifa ya kutosha kwenye fani ya *Usanii wa Picha, Chapa, Maumbo na Mapambo*. Mfano, mtahiniwa alieleza sababu za kuweka urembo kwenye nguo na bidhaa nyingine kwa kutoa hoja kama: *kuweka unamu, kuweka mizania, kuonesha mwonekano halisia n.k.* badala ya kutaja faida za kuweka urembo kwenye nguo na bidhaa nyingine kama swali lilivyotaka. Kielelezo 11.2 ni sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyepata ufaulu hafifu katika swali hili.

**Kielelezo 11.2**

11. Urembo, ni vitu vinavyovutia na kukifanya kitu /kifaa kilichotengenezwa kiweze kupendeza na kupendwa na watu mbalimbali.

Zifuatazo ni Sababu za kuweka urembo katika nguo na bidhaa nyingine;-

Ili kuleta uvutivu wa nguo na bidhaa nyingine. Urembo unapowekwa katika nguo, husaidia na kupelekea nguo kuvutia na kuonekana nzuri Hivyo nguo hiyo au bidhaa hiyo huweza kupendwa na watu mbalimbali.

Ili kuleta uhalisia wa kitu. Urembo huwekwa katika nguo na bidhaa mbalimbali ili kuleta na kuonesha uhalisia wa kitu halisi kinachowakilishwa katika bidhaa hiyo.

Ili kuweka unamu. Urembo huwekwa katika nguo na bidhaa nyingine ili kuleta ulaini na ugumu/mkwaruzo ~~wa~~ katika nguo au bidhaa hiyo. na hii husaidia watu kuipenda.

Ili kuweka mizania, Nguo na bidhaa nyingine huwekewa urembo kama vile rangi, ili kuweka mizania na kuifanya bidhaa iwe na mizania ya kuleta hali ya watu kuipenda na kuwafanya waweze kujenga ujuzi na kuchangamsha milango ya fahamu.

Urembo huwekwa ili kuonesha muonekano halisia wa nguo ~~a~~ na bidhaa nyingine. Urembo husaidia kujua uhalisia wa bidhaa kwa kutazama bidhaa au nguo husika na kujua aina ya nguo/bidhaa hiyo.


Hivyo, tunashauriwa kuweka urembo hata katika zana za kufundishia na kujifunzia ili ziweze kuwa vutivu na zenye uhalisia na kitu halisi.

Kielelezo 11.2 ni sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyeshindwa kutoa hoja zote tano sahihi na hivyo kupata alama za chini. Pamoja na hayo, mtahiniwa alishindwa kutoa hitimisho lililojitosheleza.

### 2.2.2 Swali la 12

Swali lilitoka katika mada ya *Upishi* ambalo lilimtaka mtahiniwa kufafanua faida sita za kupika chakula kwa njia ya kuchemsha. Jumla ya watahiniwa

2563 (52.9%) kati ya 4843 walifanya swali hili, ambapo watahiniwa1663 (64.9%) walipata alama 10.5 hadi 15, watahiniwa 878 (34.2%) walipata alama 06 hadi 10 na watahiniwa 22 (0.9%) walipata alama 00 hadi 5.5. Chati Na. 12 inaonesha kiwango cha ufaulu wa watahiniwa.




**Chati Na. 12** *Ufaulu wa Watahiniwa kwa Asilimia (%)*

Watahiniwa waliopata alama 10.5 hadi 15 waliweza kufafanua faida sita za kupika chakula kwa njia ya kuchemsha kwa usahihi kwa kutoa hoja kama vile: *Kutotumia gharama kubwa, kuokoa muda, ni upishi mzuri kiafya kwa kuwa mafuta hayatumiki, chakula hubaki na ladha yake ya asili* n.k. Watahiniwa hao pia waliweza kutoa utangulizi na hitimisho lililojitosheleza. Kielelezo 12.1 kinaonesha sehemu ya jibu la mtahiniwa aliyejibu swali hili kwa usahihi.

**Kielelezo 12.1**

12 Kupika chakula kwa njia ya kuchemsha ni uandaaji wa chakula ambao hautumii viungo katika kupika chakula. Katika kupika chakula kwa kuchemsha maji na chumvi tu ndo vinahitajika kuandaa zoezi la upishi. Hivyo mafuta, vitunguu na viungo vingine haviitajika wakati wa kupika chakula kwa njia ya kuchemsha. Vyakula ambavyo vinavyoweza kupikwa kwa njia ya kuchemsha ni kama vile; ndizi, magimbi, viazi na, Mihogo. Zipo faida ambazo zinatokana na upishi wa chakula kwa njia ya kuchemsha. Zifuatazo ni miongoni mwa faida hizo kama ifuatavyo:-

Haitumii gharama zaidi wakati wa kupika; kwa sababu njia hii haihitaji viungo vingi vya kupikia mfano vitunguu, karoti, nyanya na mafuta isipokuwa hutumia chumvi na maji tu hivyo huokoa gharama za kifedha za kutumika kuandalia mahitaji mengi.

Huokoa muda wa kupika. Maandalizi ya kupika chakula kwa njia kwa njia ya kuchemsha hufanyika ndani ya muda mfupi hivyo huokoa muda kwa mpishi anayeandaa chakula kwa njia hii ya upishi.

Ni njia nzuri inayoshauriwa kisayansi; Wataalamu wanashauri kwa njia ya kupika kwa kuchemsha ni bora zaidi kuliko kukaanga na kuchoma kwa sababu haitumii kemikali nyingi wakati wa kuandaliwa na kuliwa. Hivyo inapunguza kiwango cha mashambulizi ya magonjwa yanayotokana na kemikali za vyakula. Mfano kupika wali kwa kukaanga kuna viungo vingi vinawekwa wakati wa upishi ambavyo huwa na kemikali nyingi.

Kielelezo 12.1 ni sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyejibu vizuri kwa kutaja faida za kupika chakula kwa njia ya kuchemsha kama swali lilivyohitaji.

Aidha, watahiniwa waliopata ufaulu wa wastani wa alama 06 hadi 10 walitoa majibu ambayo hayakujitosheleza katika baadhi ya vipengele kutokana na kutokuwa na maarifa ya kutosha kuhusu mada husika na hivyo kupata alama pungufu. Baadhi yao walichanganya vipengele sahihi na visivyo sahihi. Mfano, mtahiniwa pamoja na kueleza baadhi ya hoja kwa sahihi, pia alieleza hoja zisizo sahihi kama *njia ya kuchemsha hutumia muda mrefu*, *chakula hupoteza ladha na baadhi ya virutubisho*, na kuwa *ni njia inayotumiwa na watu wasio na uwezo* majibu yaliyosababisha kupata alama za wastani.

Kwa upande mwingine, watahiniwa 22 (0.9%) waliopata ufaulu hafifu walishindwa kuelewa matakwa ya swali, vilevile wengine walionesha kukosa maarifa ya kutosha katika mada ya *Upishi*. Kwa mfano, mtahiniwa alitoa hoja ambazo hazikuwa na uhusiano na matakwa ya swali kama vile: *Kuupa mwili nguvu na afya*, *mwili hupata kinga ya kupambana na magonjwa*, *njia hii husaidia kuongeza ujuzi zaidi unaohusiana na upishi*, *mpishi kuwa mbunifu*, *husaidia kukuza vipaji katika upishi na kupata ajira katika hoteli* majibu ambayo hayakuwa sahihi kama inavyoonekana katika Kielelezo 12.2.

**Kielelezo 12.2**


12. Faida Zifuatazo ni faida zitokana
zo na kupika chakula kwa njia ya kuc
hemsha
Kuupa mwili nguvu na afya; kupik
a chakula kwa njia ya kuchemsha hujen
ga mwili kwa sababu vyakula vya kuche
msha huwa na virutubisho vyote vinavyo
hitajika tofauti na vyakula vingine mfan
o wa vyakula vya samaki, maboga n.k.
Husaidia mwili kuwa na kinga ya
kutosha kupambana na magonjwa; mfano
vyakula vya kuchemsha vyenye protini, wang
a n.k ambavyo ni nyama, maziwa n.k.
Husaidia kuongeza na kupata ujuzi
zaidi juu ya upishi wa vyakula vya kuche
msha mfano upishi wa vyakula vya kuche
msha mara kwa mara humfanya mtu ku
wa mzoefu na kupata ujuzi zaidi.
Humsaidia mtu anayepika vyakula
vya kuchemsha kuwa mbunifu katika njia
za kutumia kupika vyakula vya kuchem
sha.
Husaidia kuweza kukuza vipaji; ka
tika upishi kuna fani ya upishi hivyo mt
u anapokuwa hodari wa kupika vyakula
vya kuchemsha huongeza vipaji amb
avyo vinamsaidia kuwafundisha na w
engine.
Husaidia kupata ajira katika
hoteli kubwa nchini au katika familia
mbazo zinahitaji wapishi hodari wa vya
kula vya kuchemsha kama nyama au samaki.

12. Hizo ndizo faida za kupika chakula.
kwa njia ya kuchemsha ambazo ni kuwasai
dia walaji kuwa na afya bora, mwili ku
wa na nguvu n.k.

Kielelezo12.2 ni sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyechanganya maarifa kwa kufafanua faida za chakula kwenye mwili na faida za kujua upishi badala ya faida sita za kupika chakula kwa njia ya kuchemsha.

### 2.2.3 Swali la 13:

Swali lilihusu mada ya *Ususi* ambalo lilimtaka mtahiniwa kuchambua faida sita za Ususi. Jumla ya watahiniwa 4203 (86.8 %) kati ya 4843 walifanya swali hili, ambapo watahiniwa 2504 (59.6%) walipata alama 10.5 hadi 15, watahiniwa 1689 (40.2%) walipata alama 06 hadi 10 na watahiniwa 10 (0.2%) walipata alama 00 hadi 5.5. Chati Na. 13 inaonesha ufaulu wa watahiniwa kwa asilimia.




**Chati Na. 13**: *Ufaulu wa Watahiniwa kwa Asilimia (%)*

Watahiniwa waliopata alama kati ya 10.5 hadi 15 waliweza kuchambua faida za Ususi na hoja zao zilikuwa kama: *Hutangaza utamaduni wa jamii na taifa kwa ujumla*, *huibua vipaji*, *huwezesha watu kujiajiri*, *hudumisha ushirikiano* na *kukuza ubunifu*. Watahiniwa hao walionesha uwezo katika kutoa utangulizi na hitimisho lililojitosheleza. Kielelezo 13.1 kinaonesha sehemu ya jibu la mtahiniwa aliyejibu swali hili kwa usahihi

**Kielelezo 13.1**

13. Ususi ni stadi au ujuzi wa kusuka vitu mbalimbali kwa kutumia malighafi mbalimbali. Zifuatazo ni ~~sifa~~ faida za ususi.

Hukuza ubunifu, Ususi humsaidia mtu kukuza ubunifu wa kusuka vitu mbalimbali kwa kutumia malighafi au malighafi zinazopatikana katika mazingira mfano kusuka mkeka.

Ni chanzo cha ajira, kupitia stadi au ujuzi wa kusuka vitu mbalimbali humpatia mtu ajira ya kutengeneza vitu mbalimbali na kuuza ili kumwezesha kupata fedha za kumsaidia katika maisha yake.

Hutambulisha utamaduni, ususi humwezesha mtu kutambulisha utamaduni wake kupitia kazi ya ususi wa kusuka vitu mbalimbali ambavyo vinapatikana katika jamii yake mfano kusuka ~~ungo~~ nyungo.

Hukuza kipaji, Ususi humwezesha mtu kukuza kipaji chake kutoka hatua ya chini kwenda hatua ya juu mfano aliyekuwa mwususi wa vitu vidogo kama mkeka hufikia kwenda kusuka mbalimbali ambavyo vinakubalika zaidi.

Huinua kipato, ususi ni mojawapo ya mambo yanayoinua kipato cha mtu au taifa kwa ujumla kutokana na vitu ambavyo mtu husuka kwa ajili ya kuuza ili kujipatia fedha za kukidhi maisha yake.

Husaidia kupata mahitaji muhimu, kutokana na stadi au ujuzi wa kusuka vitu mbalimbali humsaidia mtu kujipatia mahitaji yake ya msingi kama vile malazi, chakula na mavazi na mahitaji mengine muhimu.

Kielelezo 13.1 kinaonesha sampuli ya majibu ya mtahiniwa aliyeweza kutaja kwa usahihi faida za ususi kama swali lilivyohitaji.

Aidha, watahiniwa waliopata alama 06 hadi 10 walitoa majibu ambayo hayakujitosheleza katika baadhi ya vipengele kutokana na kukosa maarifa ya kutosha kuhusu mada ya *Ususi* na hivyo kupata alama pungufu. Mfano, mtahiniwa licha ya kueleza vipengele vingine kwa usahihi, alichanganya hoja zingine ambazo hazikuwa sahihi kama vile: *Kuonyesha hali ya uchumi wa jamii fulani*, *kuonesha makabila yaliyo nyuma kimaendeleo* jambo lililopelekea kupata alama za wastani.

Kwa upande mwingine, watahiniwa waliopata alama 00 hadi 5.5 walishindwa kuelewa matakwa ya swali na wengine walionesha kukosa maarifa ya kutosha katika mada hii. Baadhi ya watahiniwa waliopata ufaulu hafifu walionekana kukosa stadi muhimu za namna ya kujibu maswali ya insha kwa kutoandika utangulizi na hitimisho zuri, na zaidi ya hayo kati yao wapo waliotaja hoja badala ya kuandika insha. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja alichambua faida za Ususi na kutoa maelezo ambayo hayakuwa na uhusiano kabisa na matakwa ya swali hivyo kupata ufaulu hafifu kama inavyoonekana katika kielelezo 13.2.

**Kielelezo 13.2**

13 Ususi ni kitendo cha kusuka vitu mbalimbali kwa kuzingatia kanuni na sheria zake, unaweza kusuka kwa ukili, miyaa na hata ukindu - zifuatazo ni faida za ususi nazo ni :-

Kupendezesha vitu, katika usukaji wa vitu mtu husuka ili vitu au kitu kipendeze zaidi na ndiyo maana ikamngoja makochi kupendezesha kitu.

Kuongeza gharama, pia vifaa vya ususi na ususi wenyewe humsaidia mfanya biashara ili aongeza ~~nauf~~ gharama ya kitu au vitu vyake.

Kusaidia kujipatia ajira, unapojitolea ususi unakusaidia kuwa kama nyama na sehemu ya kipaji.

Kusaidia kupata mapambo mbalimbali zaidi, watu S'addy, Shamari, ~~Chare~~ Sale. 7,00 nyingi hivyo huweza kupamba laini.

Kusaidia kuitangaza kimataifa, suala zima la ususi huifanya nchi kufahamika.

Kusaidia kuwaleta watu pamoja, ususi siku hizi ni taluma hivyo wapo watu hugiriwa kwasababu vyuo viwe wazi lakini watu huishi kwa kushirikiana.

Hivyo basi, usu~~su~~si ni taaluma ya kisayansi ambayo hulifanya taifa letu leo kuwa ~~leo~~ pamoja na ya kimataifa kwani ususi huboresha maisha ya wengi.


Kielelezo 13.2 ni sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyeshindwa kutoa maelezo yanayokidhi matakwa ya swali na hivyo kupata alama hafifu. Mtahiniwa katika hoja ya nne alitaja majina ya watu na kuongeza maneno yasiyo na mtiririko katika kutetea hoja yake.

### 2.3 Sehemu C

Sehemu C ya mtihani huu ilikuwa na maswali 3 ambapo mtahiniwa alitakiwa kujibu maswali mawili tu. Kila swali katika sehemu C lilikuwa na alama 15. Viwango vya ufaulu kwa maswali ya sehemu C (14 hadi 16) vilikuwa kama ifuatavyo: Ufaulu mzuri ulianzia alama 10.5 hadi 15, ufaulu wa wastani ulianzia alama 06 hadi 10 na ufaulu hafifu ulianzia alama 00 hadi 5.5.

#### 2.3.1 Swali la 14

Swali lilitoka katika mada ya *Ufundishaji* ambalo lilimtaka mtahiniwa kufafanua hasara sita zinazoweza kujitokeza kwa kufundisha mada ya Usanii wa Picha, Chapa, Maumbo na Mapambo bila kutumia zana za kufundishia na kujifunzia. Jumla ya watahiniwa 3950 (81.6%) kati ya 4843 walifanya swali hili, ambapo watahiniwa 3323 (84.1%) walipata alama 10.5 hadi 15, watahiniwa 615 (15.6%) walipata alama 06 hadi 10 na watahiniwa 12 sawa na 0.3% walipata alama 00 hadi 5.5. Chati Na. 14 inaonesha ufaulu wa watahiniwa waliojibu swali hili kwa asilimia.




**Chati Na. 14**: *Ufaulu wa Watahiniwa kwa Asilimia (%)*

Watahiniwa waliopata alama 10.5 hadi 15 waliweza kueleza hasara zinazoweza kujitokeza kwa kufundisha mada ya *Usanii wa Picha, Chapa, Maumbo na Mapambo* bila kutumia zana za kufundishia na kujifunzia.

Baadhi ya hasara zilizoainishwa ni pamoja na *kupunguza ari na utayari wa wanafunzi kujifunza, kutoeleweka kwa somo vizuri, kutokuwepo kwa kumbukumbu ya kudumu, muda mwingi kupotea* n.k. Watahiniwa hao walionesha kuwa na maarifa ya kutosha katika mada ya ufundishaji na uwezo mkubwa katika uandishi wa insha. Kielelezo 14.1 ni sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyeweza kujibu swali hili kwa usahihi.

**Kielelezo 14.1**

14 za kwa kufundisha mada ya "Usanii wa picha chapa, Mapambo na Maumbo bila kutumia zana za kufundishia na kujifunzia.


Wanafunzi kutofikia lengo mahsusi. Ufundishaji ambao haviambatani na matumizi ya zana unaweza kupelekea mwanafunzi kushindwa kufikia lengo mahsusi kutokana na mwanafunzi kujifunza kwa nadharia tu na siyo kwa vitendo.

Kukosekana kwa usikivu. Kufundisha mada ya Usanii wa picha, chapa, Mapambo na maumbo bila kutumia zana kunaweza kupelekea kelele darasani kutokana na wanafunzi kuvuta taswira bila kupata majibu sahihi na hivyo kuanza kuulizana wao kwa wao na kusimuliana.

Kushindwa kujengeka kwa kumbukumbu za muda mrefu. Ufundishaji wa Mada ya usanii wa picha, Mapambo, Chapa na Maumbo bila ya kutumia zana hupelekea wanafunzi kushindwa kujenga kumbukumbu za kudumu (muda mrefu) kutokana na kujifunza bila kuhusisha milango yao ya fahamu.

Wanafunzi kushindwa kufurahia somo. Ikiwa hali ya ufundishaji wa mada ya usanii wa picha, chapa, Mapambo na maumbo usipozingatia matumizi ya zana za kufundishia na kujifunzia hupelekea wanafunzi kushindwa kufurahia somo na wengi wao hutamani mwalimu amalize kuongea na hivyo aondoke kwani wanafunzi huona kama wanapotezewa muda tu.

Mwalimu kufundisha bila kujiamini. Ufundishaji wa mada ya usanii wa picha, chapa, Mapambo



14. na maumbo bila ya matumizi ya zana hupelekea mwalimu kufundisha bila kujiamini na hata kushindwa kuelezea baadhi ya dhana ngumu ambazo zinahitaji wanafunzi waone kwa macho kama vile lenzi ya kamera katika upigaji picha.

Hupelekea mwanafunzi kushindwa kujenga stadi za ubunifu na udadisi. ufundishaji usiotumia zana za kufundishia hupelekea mwanafunzi kubaki palepale alipo kutokana na kushindwa kujenga stadi za udadisi na ubunifu hii kutokana na mwanafunzi kujifunza kwa nadharia tu na siyo kwa vitendo.

Hivyo basi ili kufanikisha ufundishaji wa Mada ya Usanii wa picha, chapa, Mapambo na Maumbo Mwalimu anapaswa kuandaa zana za kufundishia ambazo zitaamsha ari ya ujifunzaji darasani na kuwafanya wanafunzi wajifunze kwa vitendo zaidi na malengo mahsusi kufikiwa kwa wakati mwafaka.


Kielelezo 14.1 ni sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyejibu swali vizuri kwa kufafanua kwa usahihi hasara zinazoweza kujitokeza endapo mada ya *Usanii wa Picha, Chapa, Maumbo na Mapambo* itafundishwa bila kutumia zana za kufundishia na kujifunzia.

Watahiniwa waliopata alama 06 hadi 10 walitoa majibu ambayo hayakujitosheleza kwa baadhi ya vipengele na hivyo kupata alama pungufu. Baadhi yao walichanganya vipengele sahihi na visivyo sahihi. Mfano mtahiniwa pamoja na kuandika hoja sahihi, alichanganya na zisizo sahihi kama vile: *Muda mwingi kupotea kwa vile mwalimu atatumia zana nyingi* na *wanafunzi watafurahia somo* ambayo ni majibu yaliyokuwa kinyume na matakwa ya swali jambo lililopelekea kupata alama pungufu.

Kwa upande mwingine, watahiniwa waliopata ufaulu hafifu kati ya alama 00 hadi 5.5, baadhi yao walishindwa kuelewa matakwa ya swali na wengine walionesha kutokuwa na maarifa ya kutosha katika mada husika. Kati yao wapo waliochanganya maarifa na kukosa stadi za namna ya kuandika utangulizi na hitimisho linaloendana na swali. Mfano, mtahiniwa alieleza faida za kufundisha mada ya "Usanii wa Picha, Chapa, Maumbo na Mapambo" kwa kutumia zana za kufundishia na kujifunzia na baadhi ya hoja alizotoa ni pamoja na *kutunza kumbukumbu ya kudumu, wanafunzi kulipenda somo, somo kueleweka vizuri* n.k. Mtahiniwa mwingine alieleza changamoto zinazoikabili fani ya *Usanii wa Picha, Chapa, Maumbo na Mapambo* kwa kutoa hoja kama *uhaba wa vifaa, uhaba wa wataalamu* n.k badala ya hasara zitakazojitokeza ikiwa mada hiyo itafundishwa pasipo kutumia zana za kufundishia na kujifunzia kama inavyoonekana katika kielelezo 14.2.

**Kielelezo 14.2**

14. Usanii wa picha, chapa, Mapambo na
Maumbo; Ni usanisi wa picha, chapa,
Mapambo na Maumbo kwa kutumia r
angi za Maji.
- Zifuatazo ni hasara za Usanii w
a picha, chapa, Mapambo na Maumbo.
Uhaba wa vifaa vya kuchore pic
ha, Mapambo na Maumbo, hii hupeleke
a uchoraji kuwa Mgumu sana. Mfano
rangi za maji pamoja na Makaratasi m
agumu.
Uhaba wa wataalamu wa kusani
si picha, chapa, Mafumbo na Maumbo,
Hii pia hupelekea ufundishaji na ujif
unzaji Mashuleni na vyuoni kuwa Mgumu
kwa sababu Mfikisha Maarifa mwenye
anashindwa kuchora.
Uwepo wa gharama kubwa, Ili
picha ivutie na ipendeze inahitaji sana
fedha, ndio maana anashauriwa Msani
andae vitu Mapema kabla hajaa
anza kusanisi picha zake.
Uhaba wa Miundo mbinu; ka



14. a vile Majengo Mabovu ambayo hayafa
poti hata ubandikaji wa picha, chapa,
Mapambo na Maumbo kwa ajili ya ufundi
shaji na ujifunzaji.
Jamii kutoona umuhimu wa usanifu w
a picha, chapa na Mapambo, Mala wanapo
kuta kwa Mfano picha zimebandikwa nak
isha upepo pia kuzipeperusha kwa Zibalo
wapo wanajamii ambao hawafahamu umuhim
u wa usani wa picha na Mafumbo huzia
cha kuzitunza vizuri.
Usani wa picha, chapa, Mapambo na
Maumbo huchafuliwa pia na wadudu, w
anyama kama vile binadamu mfano ni
Pale binadamu atakapokwenda kushika pi
cha akiwa Mikono yake ina vumbi na ni
Michafu.
Mwisho ni umuhimu wa Usanii
wa picha, chapa, Mapambo na Maumbo
Katika Ufundishaji na ujifunzaji, husaidi
a kurahisisha tendo la Ufundishaji na U
jifunzaji, hukuza udadisi pamoja na
Kujenga kumbukumbu ya Muda Mrefuk
wa wanafunzi.

Kielelezo 14.2 ni sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyeshindwa kutoa maelezo yanayokidhi matakwa ya swali na hivyo kupata ufaulu hafifu.

### 2.3.2 Swali la 15

Swali lilitoka katika mada ya *Upimaji* na lilikuwa na vipengele viwili (a) na (b). Sehemu (a) ilimtaka mtahiniwa kuchambua mambo matatu ya kuzingatia wakati wa kuandaa jedwali la utahini na sehemu (b) ilimtaka mtahiniwa kueleza faida tatu za kutayarisha jedwali la utahini katika upimaji. Jumla ya watahiniwa 1257 (26%) kati ya 4843 walifanya swali hili, ambapo watahiniwa 741 (58.9%) walipata alama 10.5 hadi 15, watahiniwa 476 (37.9%) walipata alama 06 hadi 10 na watahiniwa 40 sawa na (3.2%) walipata alama 00 hadi 5.5. Uchambuzi wa majibu ya watahiniwa katika swali hili na ufaulu wao kiasilimia umewasilishwa


katika Chati Na. 15 kwa kuonesha ufaulu wa kiwango hafifu, wastani na kizuri.




**Chati Na. 15** : *Ufaulu wa Watahiniwa kwa Asilimia (%)*

Watahiniwa waliopata ufaulu mzuri katika swali hili waliweza kuchambua vyema mambo ya kuzingatia wakati wa kuandaa jedwali la utahini na kueleza faida za kutayarisha jedwali la utahini katika upimaji kwa kutoa hoja kama vile: *kubainisha mada za upimaji*, *kubaini idadi ya maswali yanayopimwa na majazi mbalimbali ya upimaji* n.k. Aidha katika kujibu kipengele (b) kilichohusiana na faida za kutayarisha jedwali la utahini katika upimaji watahiniwa walitoa hoja kama vile: *kumwezesha mwalimu kuandaa maswali yenye uwiano*, *kumwezesha mwalimu kutathmini malengo ya somo*, *matumizi ya nyanja tofauti za upimaji* n.k. Watahiniwa katika kundi hili walionesha kuwa na maarifa ya kutosha katika mada ya Upimaji na waliweza kukidhi matakwa ya swali. Kielelezo 15.1 ni sehemu ya sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyejibu swali vizuri kwa kuchambua mambo ya kuzingatia wakati wa kuandaa jedwali la utahini na kueleza faida za kutayarisha jedwali la utahini katika upimaji.

**Kielelezo 15.1**


15. Jedwali la utahini ni jedwali lo[illegible] lo onesha maudhui na malengo yaliyo[illegible] kwa. Yafuatayo ni mambo ya kuzingatia wakati wa kuandaa jedwali la utahini

Mada ya kupima, Mwalimu anapoandaa jedwali la utahini ni lazima aweze kuainisha kuwepo na mada anayotakiwa kupima kwa wanafunzi kwa njia ya upimaji wa mazoezi, mitihani na majaribio.

Malengo ya kupima, wakati wa kuandaa jedwali la utahini mwalimu ni lazima aweze kuelewa malengo ya kupima ni yapi kwa wanafunzi

Nyanja ya utambuzi, Mwalimu ni lazima aweze kujua maarifa, ufahamu, matumizi, uchambuzi, uundaji na tathmini kwa wanafunzi wake. Zifuatazo ni faida za kutayarisha jedwali la utahini katika upimaji.

Humsaidia mwalimu aweze kutathmini maendeleo ya wanafunzi, ili aweze kupata dira na utayarishaji wa jedwali la utahini ni muhimu kwa mwalimu kuweza kutathmini maendeleo ya wanafunzi

Kielelezo 15.1 ni sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyeweza kujibu swali vizuri kwa kutoa utangulizi na ufafanuzi wa hoja kama swali lilivyohitaji.

Watahiniwa waliopata ufaulu wa wastani wa alama 06 hadi 10 walitoa majibu ambayo hayakujitosheleza katika sehemu zote (a) na (b) na hivyo kupata alama pungufu. Baadhi yao walichanganya vipengele sahihi na visivyo sahihi. Mfano katika kipengele (a), mtahiniwa alichanganya hoja sahihi na zisizo sahihi kama vile: *kutokuwa na hasira wakati wa kuandaa jedwali la utahini*, *kutotunga maswali mengi na magumu* n.k. hali iliyopelekea kupata alama pungufu.

Kwa upande mwingine, asilimia 3.2 ya watahiniwa waliopata ufaulu hafifu baadhi yao walishindwa kuelewa matakwa ya swali na wengine walionesha kutokuwa na maarifa ya kutosha katika mada ya *Upimaji*. Mfano, mtahiniwa alieleza mambo ya kuzingatia wakati wa kuandaa jedwali la utahini kwa kutoa hoja kama vile: *Kutokuwa na upendeleo kwa wanafunzi*, *kumshirikisha mwalimu mwingine* n.k hoja ambazo hazikuwa sahihi. Katika kipengele (b), mtahiniwa mwingine alitoa hoja ambazo hazikuwa sahihi kama vile: *Kujua maendeleo na nidhamu ya wanafunzi*, *hutumika kupima sehemu kubwa*, *husaidia katika kutoa motisha* n.k badala ya kueleza mambo matatu ya kuzingatia wakati wa kuandaa jedwali la utahini kama inavyoonekana katika kielelezo 15.2.

**Kielelezo 15.2**

15 Jedwali la utahini ni jedwali ambalo m
walimu hujaza taarifo za mwanafunzi katika
tabia, mwenendo, nidhamu na mambo mengine. J
edwali la utahini humsaidia mwalimu na mza
zi katika kujua maendeleo ya mwanafunzi. Wa
kati wa kuandaa jedwali la utahini kuna ma
mbo ya kuzingatia kama ifuatavyo;

Mwalimu kutokuwa na hasira wakati wa kujaza;
Wakati wa kujaza taarifa za mwanafunzi juu
ya maendeleo yake shuleni, mwalimu hautaki
wi kuwa na hasira kwa sababu unaweza kuja
za taarifa za uongo katika jedwali hilo

Kutokuwa na upendeleo kwa wanafunzi wote,
Mwalimu anapojaza taarifa za mwanafunzi
katika jedwali anapaswa asiwe na upendeleo
kwa mwanafunzi yeyote ili ajaze taarifa za
ukweli katika ~~taar~~ jedwali hilo kwa wana
funzi, wenye uwezo na wasio na uwezo, taarifa
inatakiwa ziendane na tabia au matokeo ya
mwanafunzi.

Kumshirikisha mwalimu mwingine; Wakati wa
kujaza taarifa za mwanafunzi katika jedwali
mwalimu anatakiwa amshirikishe mwenzake katik
a ujazaji kwa sababu anaweza akawa anajua
a taarifa nyingi ~~za~~ za mwanafunzi huyo hiy
o kutusaidia kujaza jedwali la utahini kw
a ufasaha na ukakika zaidi.

b)

Ufuataro ni faida za kutayarisha Jedwali la utahini katika upimaji.

Hutumika kupima schemu kubwa; ya Katika kujaza jedwali, hili la utahini usaidia kazi za kupima schemu kubwa ya mwanafunzi a wapo darasani na nje ya darasa anapokuwa akicheza na wenzake.

Husaidia kujua maendeleo na nidhamu ya mwanafunzi; Pia jedwali hili la utahini hu amsaidia mwalimu na mzazi kujua maendeleo ya mwanafunzi na tabia yake kwa ujumla akiwa darasani na katika kazi za nje ya darasa.

Husaidia katika uhuaji wa mohsha; Pia jedwali la utahini linawasaidia walimu na wazazi katika uhuaji wa mohsho kwa wanafunzi walipofaulu vizuri katika masomo yao na kufanya vizuri katika kazi za nje ya darasa.


Hivyo Jedwali la Utahini kama zana ya upimaji husaidia kuwepo na mawasiliano kati ya mzazi na mwalimu wa mwanafunzi katika shule.

Kielelezo 15.2 ni sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyeshindwa kuchambua kwa usahihi mambo ya kuzingatia wakati wa kuandaa jedwali la utahini na faida za jedwali hilo katika upimaji na hivyo kupata alama hafifu.

### 2.3.3 Swali la 16:

Swali lilitoka katika mada ya *Maandalizi ya Ufundishaji*. Swali lilimtaka mtahiniwa kuchambua vigezo sita ambavyo mwalimu anapaswa kuzingatia katika kuchagua mbinu za kufundishia na kujifunzia somo la Stadi za Kazi. Jumla ya watahiniwa 4469 (92.3%) kati ya 4843 walifanya swali hili, ambapo watahiniwa 3262 (73%) walipata alama 10.5 hadi 15, watahiniwa 1149 sawa na asilimia 25.7 walipata alama 06 hadi 10 na watahiniwa 58 (1.3%) walipata alama 00 hadi 5.5. Uchambuzi wa majibu ya watahiniwa

katika swali hili na ufaulu wao kiasilimia umewasilishwa katika Chati Na. 16 kwa kuonesha ufaulu kwa kiwango hafifu, wastani na kizuri.




**Chati Na. 16:** *Ufaulu wa Watahiniwa kwa Asilimia (%)*

Watahiniwa waliopata alama 10.5 hadi 15 waliweza kuchambua vigezo muhimu ambavyo mwalimu anapaswa kuzingatia katika kuchagua mbinu za kufundishia na kujifunzia somo la Stadi za Kazi kwa kutoa hoja kama: *umri wa wanafunzi*, *uelewa wa wanafunzi*, *ukubwa wa darasa*, *upatikanaji wa vifaa vya kufundishia na kujifunzia*, *uwezo wa mwalimu katika kutumia mbinu hizo* n.k. Watahiniwa hao walionesha kuwa na maarifa ya kutosha katika mada ya *Maandalizi ya Ufundishaji* na waliweza kukidhi matakwa ya swali. Kielelezo 16.1 ni sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyeweza kutoa jibu sahihi katika swali hili.

**Kielelezo 16.1**

16 Mbinu za kufundishia na kujifunzia ni mambo
yote anayoyafanya Mwalimu ili kuweza kumrahisi
shia ufundishaji wake anaweza kutumia mbinushi
rikishi au mbinu isiyoshirikishi. kwa sasa inasha
uliwa kabisa kwa mwalimu kuweza kutumia mbinu
inayowashirikisha wanafunzi mfano majadiliano, ka
zi mradi, bungua bongo, maswali na majibu, Vikundi
Vigezo vya kuzingatia mwalimu katika kuchagua mbinu

Umri wa wanafunzi na kiwango cha
Uelewa kwa wanafunzi hao. mwalimu lazima uzing
atie umri wa wanafunzi ambao unataka ukatumie mbi
nu hiyo mfano hauwezi kutumia kazi mradi kwa
wanafunzi wa darasa la kwanza. hivyo kiwango cha
Umri ni kigezo moja wapo cha kuchagua mbinu.

Idadi ya wanafunzi darasani. hiki ni
kigezo cha kuchagua mbinu ya kufundishia mfano
kama wanafunzi ni wachache hauwezi kutumia mbinu
ya mhadhara ambayo haimshirikishi mwanafunzi laki
ni kama ni wachache lazima uwashilikishe kwa kiwa
ngo kikubwa katika ufundishaji

Uwezo wa Mwalimu kutumia mbinu
hiyo. kabla mwalimu hajachagua mbinu lazima
aangalie anauwezo wa kutumia mbinu hiyo mfa
no mfumo wa ufundishaji wa Mwalimu mmoja
huweza kutofautiana na Mwalimu Mwingine Mfano
wengine hupenda, majadiliano, makundi, uwasilishaji
Ziara kwa hiyo kabla hujachagua lazima uangalie uwezo
weko kutumia mbinu hiyo.

Kiwango cha darasa na uelewa kwa wa
nafunzi unaoenda kuwa fundisha lazima uzing
atie hawa wanafunzi ni wadarasa gani labda
darasa la kwanza, awali, la pili au la saba, hivyo

16. kama ni awali utatumia mbinu kama nyimbo
ili mwanafunzi aweze kupenda somo unalofundisha
malengo na mada anayoenda kufun
disha kabla mwalimu hajachagua mbinu lazima uang
alie je mbinu unayochagua inaweza kufikia male
ngo uliyoya kusudiwa na mbinu hiyo itakamilisha
ujifunzaji wa mada hiyo. kwa hiyo mwalimu lazima
azingatie mada na malengo unayoenda kufundisha.
Hali ya Hewa na mazingira. lazima
Mwalimu unapochagua mbinu uangalie na Hali ya He
wa na Mazingira mfano Huwezi kwenda na wanafunzi
Mvua inanyesha kufanya Ziara, na mazingira yenyewe
mfano mjini uwambie wanafunzi wafanye kazi mradi
ya mboga mboga hivyo mbinu pia hutegemea mazingi
ra na Hali ya Hewa.
kwa hiyo ni muhimu sana Mwalimu kufua
ta vigezo vya mbinu kabla hajaingia darasani kuitumia
lakini Mwalimu anashauriwa atumie mbinu ambayo
inayowashirikisha wanafunzi katika kujifunza somo
la Stadi za kazi ambapo mbinu hizo zitazo saidia
Mwanafunzi kulipenda somo hilo kutunza kumbu
kumbu na kuvuta stadi za usikivu pindi mwalimu
anapokuwa anafundisha.

Kielelezo 16.1 ni sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyejibu swali vizuri kwa kuchambua vigezo sita ambavyo mwalimu anapaswa kuzingatia katika kuchagua mbinu za kufundishia na kujifunzia somo la Stadi za Kazi.

Aidha, watahiniwa (25.7%) waliopata ufaulu wa wastani katika swali hili, walidhihirisha mapungufu katika majibu yao, mapungufu hayo ni kama; kuchanganya hoja sahihi na zisizo sahihi, kushindwa kutoa maelezo sahihi kutetea hoja zao, kushindwa kutoa utangulizi uliojitosheleza na kurudia hoja zenye maana sawa na hivyo kupata alama pungufu.

Kwa upande mwingine, watahiniwa waliopata alama kati ya 00 hadi 5.5 walishindwa kuchambua kwa usahihi vigezo sita ambavyo mwalimu anapaswa kuzingatia katika kuchagua mbinu za kufundishia na kujifunzia. Wengi wao walishindwa kutoa utangulizi uliojitosheleza na maelezo yanayotetea hoja zao. Baadhi yao walidhihirisha kutokuwa na maarifa kabisa katika mada hii na wengine walichanganya maarifa. Mfano, mtahiniwa alieleza mbinu tofauti za kufundishia badala ya vigezo vya kuzingatia wakati wa kuchagua mbinu. Miongoni mwa hoja alizotoa ni pamoja na *kufanya ziara*, *kuajiri mwalimu mwingine ambaye ni mtaalam*, *mkusanyiko wa jopo la wataalam* na *mbinu ya majadiliano*, *kuandaa vifaa vya kutosha* n.k. Aidha, mtahiniwa mwingine alieleza faida za kutumia baadhi ya mbinu za kufundishia kama vile: *Kufanya somo lieleweke, kuwajengea wanafunzi kumbukumbu ya muda mrefu* ambayo hayakuwa majibu sahihi. Kielelezo 16.2 kinaonesha majibu ya mtahiniwa aliyeshindwa swali hili.

**Kielelezo 16.2**


16. Stadi za kazi; Ni ujuzi Mbalimbali Katika stadi Za Maisha. Nimuwana Somo hili la Stadi Za kazi liweze kufundishwa Mashuleni kwani nisomo ambalo linawajengea wanafunzi Stadi Mbalimbali Za Maisha. Zifuatazo ni Mbinu ambazo Mwalimu anapaswa kuzitumia Katika Suala nzima la Ufundishaji na Ujifunzaji wa somo la stadi Za kazi kama ifuatavyo;

Kualika Mgeni; Kama Mwalimu wa stadi Za kazi ni jambo ambalo ni muhimu katika suala nzima la kufundisha stadi za kazi ambazo Mwalimu anapaswa kutumia Kwa kualika Mgeni kwani ni mbinu ambayo ni salihi katika ujifunzaji wa somo La stadi Za kazi.

Kufanya Ziara; Pia Mbinu hii kama Mwalimu anapaswa kuitumia kwani huweza kusaidia kwa kiwango kikubwa sana na kusaidia suala nzima la ufundishaji na Ujifunzaji wa somo hili la stadi Za njia pia ni Muhimu katika kufundishia.

Kuajili Mwalimu ambaye ni Mtaalamu wa somo hili La stadi za kazi; Vilevile ni Moja ya Mbinu ambazo Mwalimu wa somo la stadi za kazi anaweza kutumia katika sula nzima la ufundishaji na uji- funzaji wa somo hili la stadi za kazi kuweza Kuajili Mwalimu ambaye ni Mtaalamu wa somo.

Kufanya Majadiliano; Vilevile hata Majadiliano ni Moja ya Mbinu ambazo Mwalimu wa stadi za kazi anapaswa kutumia kwa lengo la kurahisisha Ufundishaji.


16. Mkusanyiko wa jopo la wataalamu;
Vilevile hizi ni mapaya mbinu ambayo
Mwalimu anaweza au anapaswa kuitu
mia na kuzingatia kama moja ya mbinu
ambayo anapaswa kutumia katika
Swafanzima la kuweza kufundisha
Somo la Stadi za kazi kwani ni muhimu
katika maisha yetu ya kila siku.
Kuandaa Vifaa vya kufundisha vya ku
fundishia na kujifunzia; Zana mbali
mbali ni muhimu ziweze kuandaliwa kwa
lengo la kufundisha katika mazingira
mbalimbali ambayo watu wanaweza kukaa
na kuanza kujifunza somo hili hasta
di za kazi ni somo ambalo lina husutu
maisha yetu ya kila siku.
Kwa hiyo ni jambo ambalo ni la
muhimu kabisa kwa mwalimu kuweza
kuchagua mbinu mbalimbali ambazo zozi-
napaswa kuweza kufundisha somo-
hili la stadi za kazi kwani kuna
mbinu mbalimbali ambazo mwalimu
anaweza kuzitumia kama katika mgeni
jopo la wataalamu, na kufanya ziara.

Kielelezo 16.2 ni sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyeshindwa swali kwa kueleza mbinu tofauti za kufundishia na kujifunzia badala ya vigezo vya kuzingatia katika kuchagua mbinu za kufundishia na kujifunzia somo la Stadi za Kazi.

## 3.0 UCHAMBUZI WA KIWANGO CHA UFAULU WA WATAHINIWA KATIKA MADA

Kiwango cha ufaulu katika mada zilizotahiniwa mwaka 2018 kilikuwa kizuri ambapo 84.1% ya watahiniwa walipata wastani wa alama 40 na zaidi. Kiwango cha ufaulu cha watahiniwa katika mada za mtihani wa 634 Stadi za Kazi kinaonesha kuwa watahiniwa walifanya vizuri katika mada ya Ususi ambapo ufaulu ulikuwa ni 99.8%, Ushoni wa Nguo 99.5%, Upishi 99.1%, Maandalizi ya Ufundishaji 98.7%, Usanii wa Picha, Chapa, Maumbo na Mapambo 97.3%, Upimaji, 96.8%, Ufundishaji 92.1%, Sanaa za Maonyesho 81.7%, Misingi ya Kufundisha Somo la Stadi za Kazi 76.4%, Kilimo, Ufugaji na Uvuvi 65.7%. Aidha, kiwango cha cha ufaulu katika mada ya Muziki kilikuwa cha 18.2%.

Uchambuzi wa viwango vya ufaulu kwa kigezo cha mada katika mtihani huu unaonesha kuwa watahiniwa walifanya vizuri katika mada nyingi isipokuwa mada ya *Muziki* ambapo kiwango cha ufaulu kilikuwa 18.1%. Ufaulu wa kiwango kizuri kwa mwaka 2018 umetokana na sababu mbalimbali kama vile: watahiniwa wengi kuwa na ujuzi na umahiri wa kutosha kuhusu mada mbalimbali zilizotahiniwa na uelewa mzuri wa maswali na mtiririko wa hoja uliokidhi vigezo vya uandishi wa insha.

## 4.0 HITIMISHO

Hitimisho la uchambuzi huu limejikita katika kuangalia maswali na mada za somo la Stadi za Kazi. Kwa ujumla mtihani wa somo la Stadi za Kazi 2018 ulizingatia muhtasari wa somo husika na maeneo yote kulingana na majazi yote ya utambuzi kama vile maarifa, ufahamu, matumizi, uundaji na tathmini. Kwa ujumla kiwango cha kufaulu kwa mwaka 2018 kilikuwa kizuri kwa kuwa wastani wa kiwango hicho katika mada zote kilikuwa ni asilimia **99.92**. Aidha, uchambuzi uliofanyika unaonesha changamoto mbalimbali za watahiniwa wachache walioshindwa kufanya vizuri kama vile: uelewa mdogo wa matakwa ya swali, mtiririko usiokidhi vigezo vya uandishi, uelewa mdogo wa mada mbalimbali na uwezo mdogo katika kujibu maswali. Kadhalika, watahiniwa hao walishindwa kutoa mifano sahihi na ya kutosha katika kujenga hoja za kujibu na kutokufuata maelekezo ya swali hali ambayo iliathiri kiwango cha ufaulu wao katika somo hili.

Taarifa hii ya uchambuzi itasaidia kuinua zaidi kiwango cha ufaulu katika somo la Stadi za Kazi kwani itatoa mwongozo kwa wakufunzi na wawezeshaji katika ufundishaji wa mada zilizoonekana kuwa na matatizo. Aidha, itatoa dira kwa wanachuo na kuwahamasisha katika ujifunzaji wa mada zote za Stadi za Kazi ili kuwapa uwezo wa kufahamu vizuri fani mbalimbali zinazofundishwa kwenye somo hilo.

Aidha, taarifa hii ya uchambuzi itakuwa na tija kwa wakufunzi katika ufundishaji, utungaji na usahihishaji wa mitihani, hususani katika kuinua kiwango zaidi cha ufaulu katika somo la Stadi za Kazi ili kuendana na kauli mbiu ya Tanzania ya Viwanda na Matokeo Makubwa Sasa ya Kielimu kuwezeshwa. Taarifa hii pia inatarajiwa kutoa hamasa kwa wanachuo kuzielewa vizuri fani zinazofundishwa kwenye somo la Stadi za Kazi ili kuwapatia stadi muhimu za maisha.

Mwisho, taarifa hii ya uchambuzi kuhusu ufaulu kwa watahiniwa iwe dira katika kuwasaidia wakufunzi na wanachuo kuyaelewa makosa yaliyosababisha watahiniwa wachache kutojibu vizuri baadhi ya maswali na kisha kurekebisha kasoro hizo.

## 5.0 MAPENDEKEZO

Kutokana na uchambuzi wa maswali na mada mbalimbali za somo la Stadi za Kazi mapendekezo yafuatayo yalitolewa:

(a) Wakufunzi wahakikishe wanafundisha mada zote zilizoainishwa katika muhtasari ili kutoa maarifa na uwezo kwa wanachuo kujibu maswali kwa usahihi katika mtihani. Mfano, watahiniwa wengi walionekana kushindwa katika mada za Muziki ambayo inaonekana pengine haikufundishwa vizuri au wanafunzi hawakuielewa.

(b) Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kupitia Taasisi ya Elimu ione ni kwa namna gani somo hili linaweza kupimwa kwa mitihani ya Nadharia na Vitendo ili kuwajengea wanachuo umahiri katika stadi mbalimbali za maisha.

(c) Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kwa kushirikiana na wadau mbalimbali wa Elimu iandae warsha na mafunzo kazini ili kuwajengea wakufunzi uwezo wa kufundisha fani zote za kwenye somo la Stadi za Kazi kwa vile si vyuo vyote vyenye wataalamu wa fani zote.

(d) Aidha, kwa kuwa Serikali ya Tanzania imedhamiria kuifanya nchi kuwa ya uchumi wa viwanda, somo hili likifundishwa vizuri linaonekana kuwa chombo cha kuwezesha utekelezaji wa sera hiyo. Hivyo, ili kulipa somo uzito unaotakiwa, somo lifundishwe na kupimwa kuanzia ngazi ya shule ya msingi.

(e) Wakuu wa Vyuo wakishirikiana na wadau wengine wa elimu wahimize wakufunzi katika kuandika vitabu vya ziada na majarida ya somo la Stadi la Kazi ili kuwajengea walimu wanafunzi maarifa na umahiri katika stadi mbalimbali zinazofundishwa katika somo hili.

**Kiambatisho**

## UCHAMBUZI WA UFAULU WA WATAHINIWA KATIKA MADA

| Na. | Mada | Namba ya Swali | Asilimia ya Ufaulu | | Maoni |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | Waliopata asilimia 40 na zaidi | Wastani | |
| 1 | Ususi | 13 | 99.8 | 99.8 | Vizuri |
| 2 | Ushoni wa Nguo | 3 | 99.4 | 99.5 | Vizuri |
| 3 | Upishi | 12 | 99.1 | 99.1 | Vizuri |
| 4 | Maandalizi ya Ufundishaji | 16 | 98.7 | 98.7 | Vizuri |
| 5 | Usanii wa Picha, Chapa Maumbo na Mapambo | 1 | 95.2 | 97.3 | Vizuri |
| | | 11 | 99.4 | | |
| 6 | Upimaji | 15 | 96.8 | 96.8 | Vizuri |
| 7 | Ufundishaji | 4 | 77.2 | 92.1 | Vizuri |
| | | 6 | 92.7 | | |
| | | 8 | 98.7 | | |
| | | 14 | 99.7 | | |
| 8 | Sanaa za Maonyesho | 2 | 81.7 | 81.7 | Vizuri |
| 9 | Misingi ya kufundisha somo la Stadi za Kazi | 5 | 71.1 | 76.4 | Vizuri |
| | | 9 | 81.5 | | |
| 10 | Kilimo, Ufugaji na Uvuvi | 10 | 65.7 | 65.7 | Wastani |
| 11 | Muziki | 7 | 18.2 | 18.2 | Dhaifu |

cmyk